JAMHURI YA
MUUNGANO
WA TANZANIA

# MKEMIA NEWSLETTER

ISSN 2714-2121 | TOLEO LA 7 | JUNI 2025-JULAI 2026

Haliuzwi



# TEKNOLOJIA YA VINASABA YACHOCHEA MAENDELEO YA AFYA NA HAKI JINAI

Kamishna Jenerali aipongeza GCLA kwa kutoa matokeo ya uchunguzi kwa wakati ..................... uk 17
Mamlaka yang'ara tuzo za ubunifu katika Sekta ya Umma 2025 .............................. uk 6

# BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. Fidelice Mafumiko

**MHARIRI MKUU**
Sylvester Omary

**WAANDISHI**
1. Sylvester Omary
2. Judith Meingarai
3. Mwanaheri Jazza
4. Oscar Nkembo
5. Okello Thomas
6. Magdalena Patrick
7. Rosemary Celu
8. Mwanahija Masali
9. Regina Masolwa

**MSANIFU KURASA**
Okello Thomas



Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
5 Barabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Secherela,
Kata ya Tambukareli,
Kitalu Na 138 & 140,
Kiwanja 'AC'
S.L.P 2925, 41104 Dodoma

Tupigie
Simu: (+255) 0262161630

Barua pepe
gcla@gcla.go.tz





Karibu katika Jarida la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, chombo maalum cha mawasiliano kinacholenga kuwafikia wadau na wananchi kwa kuwapatia taarifa mbalimbali kuhusu shughuli, mafanikio, huduma na majukumu yanayotekelezwa na Mamlaka.

Jarida hili linatoa fursa kwa wasomaji kufahamu kwa karibu mchango wa Mamlaka katika uchunguzi wa kisayansi wa vielelezo vya jinai, huduma za vinasaba, udhibiti na usimamizi wa kemikali pamoja na uhakiki wa ubora wa bidhaa kwa ajili ya kulinda afya, usalama na ustawi wa jamii.

Kupitia makala, habari, mahojiano na taarifa mbalimbali, jarida hili linaendelea kuelimisha jamii kuhusu matumizi salama ya kemikali, maendeleo ya sayansi na teknolojia ya maabara pamoja na juhudi za Serikali katika kuimarisha huduma bora kwa wananchi.

Tunawakaribisha wasomaji wetu kuendelea kusoma, kujifunza na kushirikiana nasi katika kujenga jamii salama na yenye uelewa wa masuala ya kisayansi na usimamizi wa kemikali kwa maendeleo ya Taifa letu.

Asanteni kwa kuendelea kuwa sehemu ya safari yetu.




# Yaliyomo

**Ukurasa 4**

Ujumbe wa Mkemia Mkuu wa Serikali

**Ukurasa 5**

Teknolojia ya vinasaba yachochea maendeleo ya afya na haki jinai

**Ukurasa 6**

Mamlaka yang'ara tuzo za ubunifu katika Sekta ya Umma 2025

**Ukurasa 22**

GCLA yazidi kuimarisha ushirikiano na wadau wa kemikali

**Ukurasa 29**

Maafisa Polisi wapewa mafunzo ya usimamizi wa sampuli za jinai

**Ukurasa 30**

Wasimamizi na wachunguzi wa maabara watakiwa kupata mafunzo kabla ya kusajiliwa

**Ukurasa 47**

Mkemia Mkuu wa Serikali: Tafiti zetu zilenge kuhudumia jamii

**Ukurasa 49**

GCLA yaendelea kuimarisha usimamizi wa vinasaba nchini



## UJUMBE KUTOKA KWA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Ndugu wasomaji,

Kwa niaba ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, napenda kuwakaribisha katika toleo hili la jarida letu ambalo linaendelea kuelimisha, kuhabarisha na kuunganisha wadau wetu katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Jarida hili linaakisi juhudi, mafanikio na mipango inayotekelezwa na taasisi yetu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Tunaamini kuwa kupitia taarifa hizi, jamii itaendelea kupata uelewa mpana kuhusu kazi tunazozifanya pamoja na mchango wetu katika maendeleo ya taifa.

Napenda kuwapongeza wafanyakazi, wadau na washirika wetu wote kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa katika kufanikisha malengo ya taasisi. Mafanikio tunayoyaona leo ni matokeo ya mshikamano, uwajibikaji na kujituma kwa kila mmoja wetu.

Ni matumaini yangu kuwa mtaendelea kusoma na kutoa maoni yatakayosaidia kuboresha zaidi maudhui ya jarida hili katika matoleo yajayo.

Asanteni kwa kuendelea kuwa sehemu ya safari yetu ya maendeleo.

**DKT. FIDELICE MAFUMIKO**
Mkemia Mkuu wa Serikali

### DIRA

Kuwa maabara ya uchunguzi yenye hadhi duniani kwa ajili ya kushughulikia masuala ya afya, ustawi wa jamii na mazingira

### DHIMA

Kutoa huduma bora za uchunguzi wa kimaabara na udhibiti zenye ubora na gharama nafuu kwa serikali, taasisi, asasi na umma kwa ujumla kwa dhumuni la kulinda afya ya binadamu na mazingira.

### MAJUKUMU MAKUU

Majukumu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni kama yalivyoorodheshwa chini ya Sheria ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Na. 8 ya Mwaka 2016. Majukumu hayo ni:

- Kufanya shughuli za utafiti, uchunguzi wa maabara na kutoa ushauri kwa Serikali kwenye masuala yanayohusiana na uchunguzi wa sayansi jinai toksikolojia, sayansi jinai baiolojia na vinasaba, sayansi jinai kemia, vyakula, dawa usalama mahali pa kazi, kemikali za viwandani na bidhaa zake na sampuli za mazingira kwa ajili ya kutekeleza afua za afya, sheria, ustawi wa jamii na mazingira
- Kuanzisha, kusimamia na kudhibiti uendeshaji wa Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu kwa mujibu wa Sheria ya Vinasaba, Sheria ya Mamlaka na Sheria;
  Kuratibu Programu za Taifa za usimamizi wa kemikali, sayansi jinai na huduma za vinasaba
- Kusimamia Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Sumu
- Kusimamia na kuendesha mafunzo na programu za Elimu kwa Umma katika masuala yanayohusiana na usimamizi wa kemikali, huduma za vinasaba na masuala mengine yanayosimamiwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Na. 8 ya Mwaka 2016
- Kutengeneza na kutoa mwongozo, maelekezo,fursa, mafunzo na kuwaandaa wanasayansi ndani na zaidi ya utaalam wa majukumu ya Mamlaka
- Kukusanya kutambua na kuchunguza kisayansi vielelezo vinavyohusiana na masuala ya kisheria;
- Kusajili, kusitisha au kufuta maabara za kemikali, sayansi jina na vinasaba vya binadamu
- Kusajili, kusitisha au kufuta kemikali za viwandani, kemikali za majumbani au wadau wa kemikali
- Kufuta vibali vya utafiti au leseni za Vinasaba;
- Kubatilisha na kutoa maelekezo au uteketezaji wa vitu, kemikali na mazao ya kemikali
- Kumshauri Waziri kuhusu uteuzi wa wakaguzi, maafisa uchukuaji sampuli na wachunguzi wa maabara wa serikali
- Kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa maabara
- Kuchukua sampuli na kufanya uchunguzi kwenye masuala yenye maslahi ya kitafia au umma au jamii kwenye uchunguzi wa sayansi jinai, ubora wa bidhaa na usimamizi wa kemikali kadri itakavyohitajika
- Kufanya ukaguzi kwenye maeneo au huduma zinazosimamiwa na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
- Kutekeleza majukumu mengine yoyote kama atakavyoelekeza Waziri.

Gcla Tanzania/gcla_official/gcla1895
gcla_tv/www.gcla.go.tz/0800116060 (Bure)




# TEKNOLOJIA YA VINASABA YACHOCHEA MAENDELEO YA AFYA NA HAKI JINAI - Na Judith Meingarai

Serikali imesema matumizi ya teknolojia ya uchunguzi wa vinasaba yanafungua ukurasa mpya wa fursa kwa maendeleo ya jamii, nakuchochea mageuzi katika sekta ya afya, haki jinai, na uhifadhi wa rasilimali za taifa.

Akifungua maadhimisho ya Siku ya Vinasaba Tanzania 2026 yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma Aprili 23 2026, Naibu Waziri wa Afya Dkt. Florence Samizi akimuwakilisha Waziri wa Afya, Mohammed Mchengerwa, amesema kuwa teknolojia ya vinasaba imekuwa nguzo muhimu katika utoaji wa huduma za afya zenye ubora na viwango vya kimataifa.

“Katika sekta ya afya, teknolojia ya DNA imewezesha mafanikio makubwa ikiwemo utambuzi sahihi wa uhusiano wa kijenetiki katika upandikizaji wa figo na uroto, pamoja na maendeleo ya tiba za kisasa kama tiba jeni na utengenezaji wa chanjo zinazotumia mifumo ya vinasaba” alisema Naibu Waziri wa Afya.

Mbali na afya, Naibu Waziri alisisitiza mchango wa teknolojia ya vinasaba katika sekta ya haki jinai na ujangili, akibainisha kuwa ushahidi wa kisayansi unaotokana na vipimo vya maabara umeongeza ufanisi katika utoaji wa haki mahakamani, kwa kusaidia kubaini wahusika wa uhalifu au kuwaondolea tuhuma wasiohusika.

“Teknolojia hii pia imekuwa msaada mkubwa katika kutambua wahanga wa majanga na hata katika mapambano dhidi ya ujangili, kwa kubaini aina ya mnyama, jinsia na uhusika wa mtuhumiwa,” alisema Dkt.Florence.

Aidha, alisema kuwa Serikali, imeendelea kuwekeza katika miundombinu na vifaa vya kisasa ili kuimarisha uchunguzi wa vinasaba wa maabara ya kisasa yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 16 pamoja na ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchunguzi wa vinasaba.

Kwa upande wake, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, alieleza kuwa teknolojia ya vinasaba imekuwa chachu ya mapinduzi katika sekta mbalimbali ikiwemo afya, kilimo, mifugo na haki jinai, huku akibainisha kuwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imekuwa ikitumia teknolojia hiyo kwa zaidi ya miaka 20.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha Januari 2025 hadi Machi 2026 pekee, jumla ya sampuli 8,956 zilifanyiwa uchunguzi, zikisaidia kutatua masuala mbalimbali ya kijamii na kisheria.

Alibainisha kuwa hadi sasa, maabara nne zimekwishasajiliwa rasmi nchini kwa ajili ya uchunguzi wa vinasaba, huku maombi 29 ya vibali vya utafiti yakishughulikiwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

Mkutano huo, unaowakutanisha zaidi ya wataalamu 400 kutoka sekta mbalimbali, umeelezwa kuwa jukwaa muhimu la kujadili mafanikio yaliyofikiwa, changamoto zilizopo pamoja na kuweka mikakati ya kuimarisha matumizi ya teknolojia ya vinasaba nchini.

maadhimisho hayo yaliyobebwa na kauli mbiu “Kufungua Fursa kwa Jamii kupitia Uchunguzi wa Vinasaba” yamebeba matumaini mapya kwa Tanzania katika kutumia sayansi na teknolojia ya vinasaba kama nyenzo ya kuleta maendeleo endelevu, huku yakisisitiza umuhimu wa uwajibikaji, ulinzi wa taarifa na uwekezaji endelevu katika rasilimali watu na miundombinu.





# MAMLAKA YANG'ARA TUZO ZA UBUNIFU KATIKA SEKTA YA UMMA 2025 - Na Sylvester Omary

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeibuka mshindi wa Tuzo ya Ubunifu katika Sekta ya Umma, ijulikanayo kama "The Outstanding Regulatory Compliance and Safety in Chemical Management Award 2025" ikiwa ni kutambua mchango mkubwa wa Mamlaka katika mabadiliko ya usimamizi na udhibiti wa kemikali na uboreshaji wa utoaji wa huduma kwa wananchi.



Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo 16 Desemba, 2025, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amewashukuru waandaaji wa tuzo hizo na kusema tuzo hiyo itatumiwa na Mamlaka kama hamasa ya kuongeza utoaji huduma bora kwa jamii na wadau.

"Nachukua fursa hii awali ya yote kuwashukuru sana waandaaji wa hafla hii, lakini pamoja na washiriki wenzangu tunaamini kabisa tuzo hii itaendelea kutuchechemua sisi kama Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika kutoa huduma kwa jamii na kuhakikisha ubora na usalama wa bidhaa na usimamizi na udhibiti wa kemikali" alisema Dkt. Mafumiko.



Tuzo hiyo imetolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi na Uwekezaji, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hamis Suleiman Hamis, ambaye alimuwakilisha Waziri wake, Mhe. Sharrif. A. Sharrif, katika Ukumbi wa Mlimani City, Jijini Dar es Salaam, ambapo tuzo hiyo ilipokelewa na Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, ambaye aliambatana na Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo, Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Evaclotida Kapinga, Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira, Dkt. Shimo Peter na Katibu wa Mkemia Mkuu wa Serikali, Dorothy Shija.




# BODI YA TANAPA YATEMBELEA MAMLAKA

Na Sylvester Omary

Bodi ya wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Novemba 21, 2025 imefanya ziara ya kutembelea Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Makao Makuu, Dodoma kwa lengo la kujifunza namna Mamlaka inavyofanya kazi kama wadau muhimu katika masuala ya uchunguzi wa kisayansi kwa sampuli/vielelezo wanyamapori.

Wajumbe wa Bodi hiyo wakiongozwa na Mwenyekiti wake, Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali George Waitara, walipokelewa na Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, na kupewa maelezo kuhusu majukumu makuu yanayofanywa na Mamlaka yenye jumla ya maabara saba za vipimo, uchambuzi na utafiti.

Akiongea waksti wa ziara hiyo, Mwenyekiti wa Bodi, Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali, George Waitara, alisema, lengo la ziara yao ni kuweza kuifahamu Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na kutembelea maabara ya uchunguzi wa Vinasaba vya Wanyamapori.

"Ziara yetu kwa taasisi hii ina lengo la kuweza kuifahamu kulingana na majukumu yake kwa nchi na kutembelea maabara ya uchunguzi wa Vinasaba vya Wanyamapori ili kuelewa namna taratibu za uchunguzi wa kimaabara wa vinasaba kwa Wanyamapori unavyofanyika" alisema Mwenyekiti wa Bodi, Jenerali Mstaafu, George Waitara.

Naye Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, akizungumza baada ya kupokea ugeni huo amesema anashukuru kwa kutembelewa na Bodi ya TANAPA kwa sababu ni wadau wakubwa katika masuala ya uchunguzi wa Vinasaba vya Wanyamapori.

"Tumepokea ugeni huu kwa umuhimu wake kwa sababu TANAPA ni wadau wakubwa katika masuala ya uchunguzi wa kimaabara yanayohusisha Vinasaba vya Wanyamapori. Kuja kwao na kuifahamu Mamlaka itasaidia kutoa elimu kwa wadau wengine wa uhifadhi na wananchi kwa ujumla ili kufahamu taratibu za uchunguzi wa kisayansi wa sampuli na vielelezo vya Wanyamapori watakapokuwa wanahitaji kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia `Mkuu wa Serikali" alimaliza Dkt. Mafumiko.

Ziara hiyo iliambatana na kutembelea Maabara ya Vinasaba vya Wanyamapori "Wildlife DNA Laboratory" ambapo wataalam katika maabara hiyo wana jukumu la uchambuzi (Analysis Laboratory) wa vinasaba "DNA" vya wanyamapori, kutoa ushahidi wa kisayansi kwa kesi za ujangili, kutoa mafunzo juu ya ukusanyaji na uhifadhi wa sampuli/kielelezo kusimamia na kusaidia ushirikiano kati ya Mamlaka na wadau mbalimbali katika kukabiliana na masuala ya ujangili unaohusisha Wanyamapori.



*Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali George Waitara (kushoto, picha ya kwanza) wakimsikiliza Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (hayupo pichani), baada ya kutembelea Mamlaka, Makao Makuu, Dodoma, Novemba 21, 2025.*



# OFISI YA KANDA YA KASKAZINI YAKABIDHIWA NYUMBA MPAKANI - Na Okello Thomas

Katika kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali waliopo mipakani, Mamlaka imejenga nyumba za kuishi watumishi katika mipaka mbalimbali nchini ikiwemo mpaka wa Namanga, Holili, Mutukula, Rusumo na Kabanga kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi na makazi kwa watumishi.

Akizungumza wakati akikabidhi nyumba iliyopo Namanga Agosti 1, 2025, Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Evaclotida Kapinga amewataka watumishi waliopo mipakani kuzitunza nyumba hizo na kuhakikisha zinakuwa katika mazingira mazuri, safi na salama.

“Nitoe wito kwa watumishi wenzangu ambao watakuwa wanatumia nyumba hizi kwa sababu zimejengwa ili ziongeze hari ya kufanya kazi mkiwa huku mipakani na Mamlaka ipate tija kwa uwepo wa nyumba hizi. Pia niwaombe sana sisi watumishi ambao tutatumia nyumba hizi tuzione kama ni za kwetu, naomba tuzitunze na kuzilinda mali kwa ubora na kuzingatia usafi wa mazingira,” alisema Evaclotida.

Aidha, Mkurugenzi amemshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko pamoja na Menjimenti kwa kuridhia wazo la kujenga nyumba za watumishi mipakani ambazo zitawafanya watumishi wajione wenye thamani.

Akizungumza kwa niaba ya Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Msimamizi wa Huduma za Udhibiti Kanda ya Kaskazini, Joshua Mustafa ameushukuru uongozi wa Mamlaka kwa kukubali kutenga bajeti na kuwezesha kufanikisha ujenzi wa nyumba katika mpaka wa Horiri na Namanga kwani kumekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa nyumba kwa watumishi hasa zile zenye hadhi na mahitaji ya msingi.

“Hili limekuwa ni jambo kubwa sana kwetu kwani kwa sasa watumishi hasa wakaguzi watakaokuja kufanya kazi mipakani watakuwa na maeneo ya kuishi ya kudumu. Tunaamini ujenzi wa nyumba hizi utaimarisha utendaji kazi kwa wakaguzi mipakani hivyo tunatarajia kuwa na matokeo mazuri zaidi katika masuala ya usimamizi ya shughuli za Mamlaka katika maeneo ya mipaka,” alisema Joshua.



*Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi, Jerome Theogen (katikati) akiwa na watumishi wa Mamlaka, Joshua Mustafa (aliyevaa miwani) na Dismas Liwenga (kulia) wakifanya ukaguzi wa nyumba kabla ya makabidhiano yaliyofanyika katika Mpaka wa Namanga uliopo katia Wilaya ya Longido, mkoani Arusha.*



# GCLA YATAMBULIKA KIMATAIFA KATIKA UTOAJI HUDUMA - Mwanaheri Jazza, Rosemary Celu na Regina Masolwa

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imetunukiwa Cheti cha Heshima cha Forodha kwa kuthamini na kutambua mchango wake na utoaji huduma wa kipekee kwa jumuiya ya kimataifa ya Forodha.

Cheti hicho kimetolewa na Shirika la Forodha Duniani kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Forodha 2026 yaliyofanyika Januari 26, 2026, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kabla ya kukabidhi cheti hicho, Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda, ameipongeza GCLA kwa ushirikiano wake wa karibu na wa muda mrefu na TRA, inasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha ufanisi wa shughuli za forodha bandarini, kurahisisha biashara na kuimarisha udhibiti wa mapato ya Serikali.

"Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeendelea kuwa mdau muhimu na mfano wa kuigwa kwa kuzingatia misingi ya weledi, uwajibikaji na uadilifu, huku ikiendelea kushirikiana kwa karibu na TRA katika utekelezaji wa maboresho ya mifumo na taratibu za forodha kwa manufaa ya taifa" alisema Kamishna Mwenda.

Akipokea Cheti hicho kutoka kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda, kwa niaba ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa, ameishukuru TRA na Utawala wa Forodha wa Tanzania kwa kutambua mchango wa GCLA na kuahidi kuendelea kuimarisha ushirikiano uliopo ili kuongeza ufanisi wa bandari na kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Forodha 2026 yalilenga kutambua na kuenzi mchango wa sekta ya forodha katika kukuza biashara halali, kulinda uchumi wa taifa, kuongeza makusanyo ya mapato ya Serikali, pamoja na kuimarisha uwajibikaji na ushirikiano kati ya TRA na wadau wake wakuu, wakiwemo taasisi zinazosimamia bandari na biashara ya kimataifa.



*Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa (kushoto) akiwa pamoja na Msimamizi wa Dawati la Usajili na Vibali, Kanda ya Mashariki, Leocardia Magere (kulia) wakiwa na cheti kilichotolewa na Shirika la Forodha Duniani kwa kutambua mchango wa Mamlaka katika masuala ya Forodha kilichokabidhiwa na TRA katika hafla iliyofanyika ukumbi wa mlimani City Dar es Salaam Januari 26, 2026.*




# MKEMIA MKUU WA SERIKALI: ELIMU YA KEMIKALI INAWAFIKIA WADAU WETU - Na Mwanaheri Jazza

Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko, amesema elimu inayotolewa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa wadau wake kuhusu Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali imewafikia kwa kiasi kikubwa.

Dkt. Mafumiko ameyasema hayo Septemba 26, 2025 wakati alipotembelea wadau mbalimbali katika Maonesho ya Nane ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika mkoani Geita kuanzia Septemba 18 hadi Septemba 28, 2025.

"Nikiangalia Maonesho haya baada ya kutembelea na pia kuweza kuongea na Wadau wetu hususan wadau wa Kemikali, naona kuna ukuaji mkubwa sana wa uelewa wa wadau juu ya huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, zikiwemo huduma za Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali, lakini pia huduma za uchunguzi wa kimaabara.

Na kwa huduma za Usimamizi wa kemikali ukiacha tu kwamba ule ni uelewa wa wadau lakini na washiriki wanaoshiriki kwenye Maonesho haya baada ya kuongea nao unaona wanaielewa Mamlaka na hata maswali wanayouliza unaona ni ya kujenga zaidi kwa maana ya kuongeza ufanisi, lakini pia na yale masuala ya msingi yanayohusiana na mahitaji ya Sheria mengi wanayatimiza, na hii kwetu sisi kama Mamlaka ambao tunasajili na tunasimamia tunaliona kwa usalama wa watumiaji ni jambo kubwa" alisema Dkt. Mafumiko.

Kwa upande wao baadhi ya wadau wa Mamlaka, Happiness Shumbusho kutoka Jema Africa na Saad Hussein kutoka Waja Chemicals wameishukuru Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kuwapatia elimu na mafunzo mbalimbali hususan katika maswala ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali.

"Sisi kama waingizaji wa kemikali GCLA wametusaidia kwa asilimia kubwa, kwanza tumeweza kupata mafunzo ya moja kwa moja kuhusu masuala ya Udhibiti wa kemikali ambapo kwa sasa matatizo yote yanayohusiana na Kemikali hayapo, Lakini pia kwa upande wa udhibiti wa Kemikali tumekuwa tukielimishwa kuhusu kukata vibali husika na kwa muda sahihi. Pia, GCLA wametusaidia tunapoomba vibali vinakuja kwa wakati" walisema wadau hao.

Maonesho ya Nane ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yalianza Septemba 18, 2025 na kuhitimishwa Septemba 28, 2025 huku yakibeba kauli Mbiu Isemayo "Ukuaji wa Sekta ya Madini ni Matokeo ya Matumizi ya Teknolojia sahihi na Uongozi Bora, Shiriki Uchaguzi Mkuu 2025.



*Mtumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Hadija Makurunge (kulia), akitoa elimu kuhusu majukumu mbalimbali ya Mamlaka kwa wananchi na wadau waliotembelea banda la Mamlaka.*



# WADAU WASISITIZWA MATUMIZI SALAMA YA KEMIKALI - Na Sylvester Omary

Meneja wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, Eliamini Mkenga, amewataka wasimamizi na watumiaji wa kemikali kutumia kwa uangalifu kwa sababu hakuna kemikali rafiki kwa binadamu na mazingira.

Meneja Mkenga amesema hayo Desemba 2, 2025 wakati akifungua mafunzo ya usimamizi salama wa kemikali kwa wasimamizi wa kemikali kutoka mkoani Arusha.

"Hakuna kemikali rafiki kwa binadamu, kila moja ina madhara kwa binadamu kama itatumiwa tofauti na inavyotakiwa kulingana na maelekezo yake. Hivyo tunahitajika kuwa waangalifu na makini tunapotumia na kuzisimamia kemikali za aina yoyote. Mafunzo haya yatawasaidia kuweza kufahamu namna ya kutunza, kusafirisha na kujikinga ili kutoweza kupata madhara ya kemikali mnapokuwa mnazitumia na kuzisimamia" alisema Mkenga.

Aidha, alieleza kwamba Sheria inawataka kutoa mafunzo kwa wasimamizi na watumiaji wa kemikali mara kwa mara ili kuongeza umakini na kuchukua tahadhari ya matumizi ya kemikali kwenye maeneo ya kazi.

"Lazima tuzingatie taratibu za usalama wa matumizi ya kemikali ili kuepusha ajali na madhara yanayoweza kusababishwa na kemikali zisiposimamiwa kikamilifu" alimaliza Meneja Mkenga.

Naye mshiriki wa mafunzo hayo kutoka kampuni ya Gasco, Lucas Godfrey, akizungumza kuhusu mafunzo hayo alisema mtazamo wao mkubwa walionao ni kwamba mafunzo hayo yatawaongezea uelewa katika matumizi ya kemikali lakini pia kujua mabadiliko na maboresho ya miongozo na sheria ya kemikali ili kuhakikisha wanawajibika katika usimamizi wa kemikali.

"Mafunzo haya ni sehemu ya kuboresha katika mapungufu tuliyonayo hususani katika eneo la kemikali kwenye uhifadhi na matumizi lakini pia kufikisha elimu hii kwenye maeneo yetu ya kazi na jamii husika" alimaliza Godfrey.



*Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kaskazini, Eliamini Mkenga (aliyesimama katikati, akiwa pamoja na wawezeshaji na washiriki wa mafunzo ya usimamizi salama wa kemikali mara baada ya kufungua mafunzo hayo yanayofanyika katika hoteli ya Corridor Spring, jijini Arusha, Desemba 2, 2025.*




# WATUMISHI WAPYA WAASWA KUFUATA UTAMADUNI

Na Okello Thomas

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amewataka watumishi wapya na waliohamia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhakikisha wanaelewa majukumu ya Mamlaka na utamaduni wake ili iwawezeshe katika utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi.

Dkt. Mafumiko alisema hayo alipokuwa akifungua mafunzo ya awali kwa waajiriwa wapya na watumishi waliohamia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali yaliyofanyika Dar es Salaam Julai 28, 2025.

“Kila taasisi ina majukumu na utamaduni tofauti na taasisi nyingine, hivyo kutokana na sababau hiyo Mamlaka imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wote wanaojiunga na Mamlaka kwa njia ya ajira mpya au uhamisho kwa lengo la kuwafahamisha majukumu na utamaduni wa taasisi hii,” alisema Mkemia Mkuu wa Serikali.

Pia, Dkt. Mafumiko aliongeza kuwa mafunzo hayo yatawawezesha watumishi hao kuijua vyema Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa maana ya majukumu yake nyeti kwa Serikali na jamii ya Watanzania lakini pia watajifunza umuhimu wa utunzaji wa siri ambao ni moyo wa utendaji wa Mamlaka.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Evaclotida Kapinga, aliwasihi watumishi wapya kuwa wasikivu kwa kipindi chote cha mafunzo na pia wawe huru kuuliza maswali pale inapolazimu ili kwa pamoja waweze kuelewa namna shughuli zinavyofanyika kwenye taasisi.

Mafunzo hayo yamewezeshwa na wawasilishaji mbalimbali kutoka ndani ya taasisi, wataalam kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) pamoja na wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.







## WATUMISHI WAASWA KUJENGA UTAMADUNI WA KUFANYA MAZOEZI - Na Judith Meingarai

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko amewataka watumishi wa Mamlaka kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi na michezo ili kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza na kuimarisha afya zao.

Mkemia Mkuu wa Serikali ametoa rai hiyo Julai 19, 2025 wakati wa ufunguzi wa Bonanza la watumishi wa Mamlaka, takribani 190 kutoka Makao Makuu, Dodoma na Ofisi ya Dar es Salaam lililofanyika katika eneo la Ndoto Pole pole lililopo Mapinga, Bagamoyo.

"Michezo husaidia kuboresha afya na kujenga mahusiano mazuri kati ya watumishi. Utekelezaji Mzuri wa majukumu yetu ya kila siku hutegemea sana afya ya mwili na akili" alisema.

Aidha, Dkt. Mafumiko, alisema kuwa kupitia michezo watumishi hupata burudani na kupunguza msongo wa mawazo unaoweza kusababishwa na kukosa nafasi ya kufanya mazoezi au kushiriki michezo mbalimbali.

Hata hivyo, alieleza lengo la bonanza hilo kuwa ni kuwapa washiriki fursa ya kufarahia burudani mbalimbali katika mazingira yasiyo rasmi ya kikazi, ili kusaidia kupumzisha akili na kuongeza ari ya utendaji, kuwezesha ushiriki wa michezo na shughuli za mazoezi kwa lengo la kuimarisha afya ya mwili na akili na kutoa jukwaa la kubadilishana mawazo na uzoefu.

Naye mmoja wa watumishi wa Mamlaka kutoka Makao Makuu Dodoma, Msafiri Mwasyeba, alimshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na Menejimenti ya Mamlaka kwa kuweza kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili bonanza la michezo kwa watumishi.



*Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, akifungua Bonanza la watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Makao Makuu lililofanyika katika eneo la Ndoto Pole pole, Mapinga Bagamoyo mkoani Pwani Julai 19, 2025. Kulia ni Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira, Dkt. Shimo Peter.*





Gcla Tanzania/gcla_official/gcla1895
gcla_tv/www.gcla.go.tz/0800116060 (Bure)



# GCLA YAPONGEZWA KWA KUWA CHACHU YA UPATIKANAJI WA WANASAYANSI TANZANIA - Na Oscar Nkembo

Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara ya Afya, Dkt. Hamad Nyembea, ameipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kutoa tuzo kwa Wanafunzi na Walimu bora zaidi kitaifa wa masomo ya sayansi katika mitihani ya kidato cha nne mwaka 2023 na kidato cha sita mwaka 2024.

Dkt. Nyembea aliyasema hayo Juni 12, 2025 akimuwakilisha Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama, katika hafla ya kuwatunuku tuzo Wanafunzi na Walimu bora zaidi wa somo la Fizikia, Kemia, Baiolojia na Hisabati kidato cha nne 2023 na kidato cha sita 2024, iliyofanyika katika ukumbi wa Golden Jubilee jijini Dar es Salaam, ambapo amesema kuwa tuzo hizo zina tija kubwa kwani ni chachu na zinadhihirisha kutambua umuhimu wa masomo ya Sayansi na kuhamasisha vijana kupenda masomo ya Sayansi.

"Tukio hili lina tija kubwa sana kutokana na uwepo wa majanga mbalimbali ya kidunia ambapo watalamu wa Sayansi wamekuwa na mchango mkubwa katika kuyapatia ufumbuzi, na katika Serikali ya awamu ya sita wataalamu hawa wanahitajika kwa wingi kwenye sekta ya Afya na suala la kupata wataalamu hawa halina mbadala" alisema Dkt. Nyembea.

Katika hatua nyingine Dkt. Nyembea alisema Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka mazingira wezeshi kwa kujenga Madarasa, Maabara na kuajiri Walimu ili wanafunzi wa masomo ya Sayansi waweze kufanya vema na Taifa letu liweze kupata wataalamu wa kutosha.

kujenga Madarasa, Maabara na kuajiri Walimu ili wanafunzi wa masomo ya Sayansi waweze kufanya vema na Taifa letu liweze kupata wataalamu wa kutosha.

Naye Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, alisema lengo la tuzo hizo ni kujenga hamasa ya kupenda masomo ya Sayansi kwa kuwa yana mchango mkubwa sana katika Taaluma ya Afya ambayo wataalamu wake wanatokea katika masomo mama ya Sayansi ambayo ni Fizikia, Kemia, Baiolojia na Hisabati ambapo kwa mwaka 2025 tuzo zimetolewa kwa masomo hayo yote.

Nao Judith Haule na Joselini Johanes ni wanafunzi ambao wamepata tuzo hizo, wameishukuru Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kuwatambua na kuwaongezea hamasa ya kufanya vizuri zaidi na hatimaye kulitumikia Taifa baada ya kuhitimu Taaluma mbalimbali.

"Tunaishukuru sana Mamlaka kwa sababu wamefanya kazi kubwa kuanzia wazo lao mpaka kututafuta nchi nzima kiukweli Mamlaka hii imetutia moyo sana na tunajihisi kuwa na deni kwa Taifa letu" walisema wanafunzi hao.



*Wanafunzi waliofanya vizuri zaidi, wakiwa katika hafla ya kuwatunuku tuzo Wanafunzi na Walimu bora zaidi wa somo la Fizikia, Kemia, Baiolojia na Hisabati waliohitimu kidato cha nne mwaka 2023 na kidato cha sita 2024. Hafla hiyo imefanyika katika ukumbi wa Golden Jubilee jijini Dar es Salaam Juni 12, 2025.*



# KANDA YA ZIWA YATOA MAFUNZO KWA WAJASIRIAMALI

Na Okello Thomas

Wajasiriamali wadogo kutoka mkoani Mwanza wameahidi kubadili mbinu za uzalishaji wa bidhaa zinazotumia kemikali kwa kutumia vifaa vya kisasa na vifaa kinga kwa lengo la kufuata misingi ya sheria ya kemikali..

Wajasiriamali walisema hayo baada ya kupata mafunzo ya matumizi salama ya kemikali yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kupitia Ofisi ya Kanda ya Ziwa yaliyofanyika katika ukumbi wa TMDA jijini Mwanza Januari 12, 2026.

Akizungumza kwa niaba ya Wajasiriamali, Ruth Mfanga, amesema kuwa baada ya kupata elimu hiyo, Wajasiriamali wamejipanga vyema kuhakikisha wanaenda kufanya kazi kwa kuzingatia usalama wa afya na mazingira huku wakitumia vitendea kazi vya kisasa kwenye kuchanganya kemikali.

"Elimu hii tuliyoipata imekuwa mwanga katika maendeleo ya shughuli zetu za ujasiriamali kwa kutuongezea maarifa kwenye utumiaji wa kemikali. Pia, tunaishukuru Mamlaka kwa kutoa elimu kwa wajasiriamali na tunaomba hii elimu iwe endelevu na iwafikie wadau wengi zaidi huku na sisi tutakuwa mstari wa mbele kuelimisha jamii pamoja na wafanyabiashara wenzetu ambao bado hawajapata elimu," alisema Ruth.

Kwa upande wake Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Ziwa, John Wanjala, alisema kuwa mafunzo hayo yatapelekea kuwa na idadi kubwa ya wadau wa shughuli za kemikali wenye weledi wa kusimamia vyema shughuli za kemikali na hivyo kuimarisha jitihada za Serikali za utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani namba 3 ya mwaka 2003, na Kanuni zake za mwaka 2020.

Naye, Afisa Biashara Mwandamizi kutoka Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo (SIDO), Maneno Maporo, ameipongeza Mamlaka kwa kuendeleza ushirikiano na SIDO kwani imeweza kuleta wajasiriamali pamoja na kuwapa elimu ili waweze kufanya shughuli zao kwa kufuata misingi ya Sheria.



*Washiriki wa mafunzo ya matumizi salama ya kemikali wakifuatilia mada mbalimbali zilizowasilishwa na wawezeshaji kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Ofisi ya Kanda ya Ziwa.*



Gcla Tanzania/gcla_official/gcla1895
gcla_tv/www.gcla.go.tz/0800116060 (Bure)



# WATAALAM WA MAABARA WAHIMIZWA KULINDA ITHIBATI

Na Okello Thomas

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imetoa mafunzo ya utekelezaji wa mifumo ya ubora ya maabara (ISO/IEC 17025:2017) kwa wataalam wa maabara kwa lengo la kuongeza umahiri katika utendaji wa kila siku katika maabara, kuongeza umahiri kwa watumishi, kuimarisha hadhi ya maabara za Mamlaka kulingana na Viwango na matakwa ya Kimataifa pamoja na kuiwezesha Mamlaka kuongeza wigo wa Ithibati katika Maabara zake.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika Januari 5 hadi 9, 2026 kwenye Chuo cha Ustawi wa Jamii, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko alisema kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 kinaipa maabara uwezo wa kuonesha umahiri wake katika kufanya uchunguzi na kutoa matokeo ya maabara yanayotambulika na kukubalika kitaifa na kimataifa, na utekelezaji wa kiwango hicho si hitaji la ithibati pekee, bali ni nyenzo muhimu ya kuimarisha ubora, uaminifu na ushindani wa huduma za maabara.

"Nitumie fursa hii kusisitiza kwamba juhudi na uwajibikaji wenu ndiyo msingi wa mafanikio ya ithibati katika Mamlaka. Mafanikio ya Maabara kupata ithibati na kuitekeleza kwa vitendo yatatoa sifa njema si tu kwa Mamlaka bali pia kwa Taifa kwa ujumla. Aidha, Mamlaka itaendelea kutoa rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa ubora ulioanzishwa kulingana na mahitaji ya viwango vya Ubora wa Kimataifa (ISO)," alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, Mkemia Mkuu wa Serikali alitoa msisitizo kwa watumishi wote wa Mamlaka kuhusu umuhimu wa kuwajibika binafsi na kujitambua kitaaluma, hususan kadri mtu anavyozidi kupata uzoefu katika maeneo yake ya kazi kwani uzoefu wanaoupata si mali ya mtu binafsi pekee, bali ni rasilimali muhimu ya Taasisi inayopaswa kushirikishwa na kuendelezwa kwa makusudi ili kujenga uwezo endelevu wa Mamlaka.

Kwa upande wake Mwezeshaji kutoka Umoja wa Maabara, Bi. Kezia Mbwambo alisema kuwa Kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 ni mfumo wa usimamizi uliotengenezwa na Shirika la Viwango vya Kimataifa (ISO) linalolenga seti ya mahitaji ambayo Taasisi au Shirika linapaswa kufikiakatika mfumo wa ubora ili kupata hati ya ISO.

Naye Riphat Lusingo, ameishukuru Mamlaka kwa kuwezesha mafunzo hayo na kuahidi kwa niaba ya wataalam wote wa maabara kuendelea kujituma katika kutekeleza mifumo ya ubora kwa kuzingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya maabara, kutekeleza taratibu, miongozo na nyaraka za maabara kwa hiari na uwajibikaji.



*Mwezeshaji wa mafunzo kutoka Umoja wa Maabara Tanzania, Kezia Mbwambo, akitoa elimu juu ya mifumo ya ubora kwa wataalam wa maabara kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.*




# KAMISHNA JENERALI AIPONGEZA GCLA KWA KUTOA MATOKEO YA UCHUNGUZI KWA WAKATI - Na Okello Thomas

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiboresha Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali hali iliyochochea utolewaji wa majibu ya uchunguzi wa kimaabara kwa wakati.

Kamishna Jenerali Lyimo, alisema hayo Julai 5, 2025 wakati alipotembelea banda la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika maonesho ya 49 ya kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam "Sabasaba" yanayofanyika katika viwanja vya Maonesho Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam.

"Tunaishukuru Serikali ya `awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuiboresha Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kununua vifaa vya kisasa ambapo sasa hivi unapopeleka sampuli mbalimbali unapata majibu kwa wakati jambo linalorahisisha kupeleka mashtaka mahakamani kwa haraka na kusaidia haki kuweza kupatikana" alisema Lyimo.

Katika hatua nyingine Kamishna Jenerali amemshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kutoa ushirikiano mkubwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwani ndiye mdau mkubwa wa kuweza kukamilisha majalada ya Mamlaka hiyo.

"Tunamshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kutupa ushirikiano mkubwa kwani ndiye mdau mkubwa wa kuweza kukamilisha majalada ya Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya kwasababu ili kesi iweze kukamilika ni lazima tupate cheti kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali, na tunashirikianae katika oparesheni mbalimbali za kupambana na kudhibiti dawa za kulevya" alisema Lyimo.

Naye Mkurugenzi wa uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira, Dkt Peter Shimo, ameishukuru Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa ushirikiano mkubwa inaotoa kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kukamilisha mnyororo wa haki Jinai katika upatikanaji wa haki kwa wakati.

"Tunashukuru kwa ushirikiano mkubwa tunaopata kutoka DCEA kwani ni jukumu letu sote katika mnyororo ule wa haki Jinai, tunaendelea kuwekeza katika mitambo na kuboresha mbinu za uchunguzi na tunaishukuru Serikali kwa kutuongezea watumishi na kuwekeza katika Taaluma zao ili kuongeza ufanisi katika utendaji" alisema Dkt. Shimo




*Mtumishi wa Mamlaka (kulia) akitoa elimu kuhusu majukumu ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa wananchi waliotembelea banda la Mamlaka.*



# MKEMIA MKUU WA SERIKALI AWATAKA WAJUMBE WA BARAZA KUWAJIBIKA - Na Okello Thomas

Mkemia Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanayakazi la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amewataka watumishi wa Mamlaka kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika sehemu zao za kazi ili tija iweze kuonekana katika utekelezaji wa majukumu yao.

Akazungumza wakati akifungua Kikao cha Pili cha Baraza la Nane la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kilichofanyika Oktoba 23, 2025 katika mkoani Morogoro, Mkemia Mkuu wa Serikali amewakumbusha watumishi wa Mamlaka kuendelea na utamaduni wa kufanya kazi kwa weledi na ufanisi ili kufikia malengo ya taasisi.

"Ni wajibu wa kila mtumishi kufuata misingi ya kazi na endapo mtaamua kutekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia weledi, ufanisi na uwajibikaji, ni dhahiri kuwa tija itaonekana kazini," alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, Mkemia Mkuu wa Serikali amebainisha kuwa jukumu la msingi la Baraza la Wafanyakazi ni kushauri Menejimenti katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ambayo taasisi inawajibika kwa umma na kujadili bajeti ya taasisi na utekelezaji wake kwa kila mwaka wa fedha. Pia, ametoa rai kwa wajumbe wa Baraza la wafanyakazi la Mamlaka kutumia nafasi ya uwakilishi kwa kutetea na kulinda haki kwa maslahi ya watumishi na taifa kwa ujumla.

"Maamuzi yanayopitishwa ndani ya Baraza hili ni kwa ajili ya maslahi ya taasisi, hivyo, wajumbe tulioko hapa kwa uwakilishi tuendelee kuwahamasisha wenzetu kwa kuwapa mrejesho kutokana na maamuzi tuliyofikia," aliongeza Mkemia Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TUGHE, tawi la Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Adam Mbugi, amempongeza Mkemia Mkuu wa Serikali, Bodi pamoja na Menejimenti kwa mahusiano mazuri na Wafanyakazi na ushirikiano wa pamoja hali inayopelekea Baraza kuwa la usikivu na uwazi.

Pia, Mjumbe wa Balaza la Wafanyakazi la Mamlaka, Martha Msola, amepongeza Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka, Dkt. Fidelice Mafumiko, kwa ambavyo amekuwa akiongoza Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka kwa kutoa demokrasia y hali ya juu kwa Wajumbe kuweza kutoa maoni na ushauri.



*Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka, Dkt. Fidelice Mafumiko (katikati) akiwa pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka katika siku ya kwanza ya kikao cha pili cha Baraza la Nane la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kilichofanyika katika ukumbi wa Cate Hotels, Morogoro Oktoba 23, 2025.*



# KEMIKALI NI MUHIMU KWA AFYA NA UCHUMI

Na Judith Meingarai

Wadau wa Kemikali wameelezwa kuwa usimamizi na udhibiti salama wa kemikali ni msingi muhimu wa kulinda afya ya jamii, mazingira, usalama wa Taifa na kukuza uchumi wa nchi.

Akifungua Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa Kemikali kwa mwaka 2026 lililofanyika Hoteli ya Cate, mkoani Morogoro, Januari 22,2026, Mgeni Rasmi, Dkt. Hamad Nyembea aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya alisema kemikali ni nguzo muhimu ya maendeleo ya sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo afya, viwanda, kilimo, madini na usafirishaji.

"Hatuwezi kujadili maendeleo ya nchi yetu bila kutambua mchango mkubwa wa kemikali, kwani ni injini ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii," alisema Dkt. Nyembea.

Aliongeza kuwa pamoja na mchango wake mkubwa, kemikali lazima zitumike kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo ili kuepuka madhara kwa jamii na mazingira.

"Ukuaji wa biashara ya kemikali lazima uende sambamba na ulinzi wa afya ya jamii, mazingira na usalama wa nchi. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendekezo na maazimio yatakayotolewa katika jukwaa hilo kwa lengo la kuimarisha sekta ya kemikali nchini" alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, alisema jukwaa hilo limewakutanisha zaidi ya washiriki 250 kutoka sekta ya umma na binafsi, wakiwemo waingizaji, wasafirishaji, watunzaji na watumiaji wa kemikali.

jukwaa hilo limewakutanisha zaidi ya washiriki 250 kutoka sekta ya umma na binafsi, wakiwemo waingizaji, wasafirishaji, watunzaji na watumiaji wa kemikali.

"Jukwaa hili limeweka mfumo shirikishi unaowakutanisha Serikali na Sekta Binafsi ili kujadili kwa pamoja biashara, matumizi na usimamizi wa kemikali nchini," alisema Mkemia Mkuu wa Serikali.

Alibainisha kuwa kupitia jukwaa hilo, wadau wanapata fursa ya kujadili mchango wa kemikali katika uchumi wa Taifa, changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya kuhakikisha sekta hiyo inakua kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182.

"Lengo letu ni kuhakikisha ukuaji wa sekta ya kemikali unakwenda sambamba na ulinzi wa afya, mazingira na usalama wa nchi," aliongeza.

Akizungumza kwa niaba ya wadau wa kemikali, Abdallah Kingulilo, alisema wadau wamefurahishwa na utambuzi wa Serikali kwa sekta hiyo kama nguzo muhimu ya uchumi wa taifa. Aliishukuru Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ushirikishwaji wa wadau, akisema jukwaa hilo ni fursa ya kujadili changamoto na kutoa ushauri wa pamoja kwa maendeleo ya taifa.




*Mwakilishi wa Katibu Mkuu, na Mkurugenzi wa Tiba, Wizara ya Afya, Dkt Hamad Nyembea (aliyekaa katikati) akiwa na viongozi wa Mamlaka pamoja na washiriki wa Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa Kemikali kwa mwaka 2026 baada ya kufungua mkutano huo wa siku mbili unaofanyika katika ukumbi wa Cate Hoteli, Morogoro, Januari 22, 2026.*




# MAMLAKA YATAKIWA KUTHIBITI UBORA WA TIBA ASILI

Rosemary Celu na Mwanahija Masali

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imetakiwa kusimamia na kuthibiti Ubora na Usalama wa Huduma za Tiba asili nchini, ili kujenga Imani kwa Umma kupitia viwango na weledi kwa kufuata sheria, maadili na vigezo vya kuzalisha na kusambaza dawa za Tiba Asili.

Akizungumza katika Mkutano wa Wataalam wa Tiba Asili Machi 25, 2026 jijini Dodoma, Waziri wa Afya, Mhe. Mohammed Mchengerwa, alisema kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali anao umhimu mkubwa wa kuthibitisha ubora na usalama wa huduma za Tiba Asili.

"Sambamba na hilo ni wajibu wetu kujenga imani ya umma kupitia viwango, hatuondoi utamaduni wetu wa Tiba Asili tunaupa uweledi na tunawekea mifumo na tuna uhifadhi kwa kufuata sheria, maadili na vigezo vya ubora ndio maana usimamizi wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, TMDA, Mkemia Mkuu wa Serikali, NIMR, na taatisisi za Tiba Asili, MUHAS, mnao umuhimu mkubwa wa kuthibitisha Ubora na usalama wa bidhaa na huduma hizi," alisema Mchengerwa.

Naye Kaimu Meneja Maabara ya Maikrobaiolojia, Alois Ngonyani, amesema kuwa wanaendelea kukutana na Wataalamu wa Tiba Asili na kuwapa elimu na mbinu mbalimbali za uchukuaji wa Sampuli salama ili kuhakikisha wanapata majibu sahihi na ya kuridhisha ambayo yamezingatia uchukuaji mzuri wa Sampuli.

"Tumepanga wakati wa mafunzo kuchukua sampuli mia moja kwa ajili ya kuzifanyia uchunguzi wa kimaaabara na tuweze kutoa majibu na kuzisaidia Mamlaka za maamuzi ambalo ni baraza la tiba asili liweze kufanya maamuzi kuhusiana na hizo dawa," alisema Ngonyani.

Aidha Mtaalam na mtumiaji wa Dawa za Tiba Asili, Emily Kombe, amewashauri watanzania kuwa wazalendo kutumia Dawa za Asili na kuachana na imani potofu ikiwemo wengi wao kuwa na dhana ya kuwa ni imani za kishirikina ambapo inawawia ugumu wataalam hao kupata soko katika bidhaa zao.

"Huwa Napata changamoto kwa watu wanaoumwa ukimpelekea Dawa hasa kwa Wachungaji anafikiri kuna vitu flani vinachanganywa, Hapana hiyo ni imani potofu yaani hizi hapa ni tofauti kabisa na wale waganga wanaopiga ramli, hizi ni dawa ambazo hazina mambo ya kishirikina hivyo wasiwe na wasiwasi kuzitumia maana ni miti shamba, haina kemikali na ina faida kubwa sana mwilini," alisema Kombe.




*Kaimu Meneja wa Maabara ya Maikrobaiolojia, Alois Ngonyani (aliyevaa kofia) akitoa Elimu kwa Wataalamu wa Tiba Asili walipotembelea Banda la Mamlaka kwenye kikao cha Waziri wa Afya na wataalam wa Tiba Asili kilichofanyika Mtumba, Dodoma.*



## BENSON 'MWAKANI TUTAFIKA NUSU FAINALI'

Na Oscar Nkembo

Kocha Mkuu wa Timu ya Mpira wa Pete ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Benson Mkwama, amesema kama ataendelea kuwa kocha wa timu hiyo kwa msimu ujao atahakikisha timu hiyo inafika nusu fainali ya michuano ya SHIMMUTA.

Kocha Benson alisema hayo Desemba 3, 2025 baada ya kumalizika kwa mchezo wa robo fainali ya mashindano ya SHIMMUTA na kufungwa mabao 46-22 dhidi ya Chuo Kikuu Cha Dodoma katika mchezo uliofanyika katika uwanja wa Bwalo mkoani Morogoro.

"Nilitamani tufike robo fainali na tumefikia nadhani ni hatua nzuri kwa uwezo wa wachezaji wetu na tumekutana na mpinzani ambaye ametuzidi uwezo na uzoefu, mwakani tunakuja tukiwa timu kubwa jambo la msingi tujiandae vizuri na kama nitaendelea kuwepo kwenye timu nitahakikisha timu hii inafika nusu fainali" alisema kocha Benson.

Kwa upande wa Nahodha wa Timu, Victoria Kyara, amesema mashindano yalikuwa magumu sana lakini mapambano ndio yameleta mafanikio haya.

"wachezaji wamepambana sana haya mashindano sio rahisi, nakumbuka misimu miwili iliyopita tuliishia hatua ya 16 bora na msimu huu tumefika robo fainali naamini msimu ujao tutakuwa bora zaidi" alisema Victoria Kyara.

Aidha, Sholastica Hyera, amemshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali na Menejimenti ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kutoa ruhusa ya kushiriki katika michuano hiyo.

"Tunamshukuru sana Kiongozi wetu Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kuturuhusu kuja kushiriki mashindano haya na hatujatosheka kwa kufika robo fainali tumepata somo na lengo letu ni kutwaa ubingwa wa netball" alisema Sholastica.








## GCLA YAZIDI KUIMARISHA USHIRIKIANO NA WADAU WA KEMIKALI - Na Okello Thomas

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Kisirye Ukio, alitoa rai kwa wadau wa kemikali kuzingatia Sheria na Miongozo zinazosimamia masuala ya kemikali ili kuepuka madhara kwa afya ya binadamu, wanyama na mazingira kwani madhara huweza kutokea endapo sheria zisipozingatiwa.

Mganga Mkuu alitoa rai hiyo wakati akifunga mafunzo ya mwaka ya uimarishaji kwa wasimamizi wa kemikali yaliyofanyika kwa siku 3 kuanzia Desemba 1 hadi 3, 2025 katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Julius Nyerere Kibaha mkoani Pwani.

"Ni jukumu lenu kuhakikisha mnakuwa mstari wa mbele kulinda afya zenu, za wengine pamoja na mazingira na ili haya yote yatimie, mnatakiwa kuwa mabalozi wa kueneza elimu ya matumizi yaliyo sahihi na salama ya kemikali," alisema Ukio.

Pia, ameisihi Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali iendelee kutoa elimu ya madhara ya kemikali kwa kuwafikia wadau mbalimbali wa kemikali pamoja na wananchi wa kawaida.

Kwa upande wake Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa, amewapongeza washiriki wa mafunzo hayo kutoka kwenye kampuni binafsi, taasisi za Serikali na kuwataka waendelee kutoa ushirikiano kwa Mamlaka jambo ambalo litasaidia katika kutekeleza Sheria zinazosimamiwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Pia, Mkapa ameongeza kuwa kupitia mafunzo hayo Mamlaka imepata mafanikio makubwa ya kuwa karibu na wadau wa kemikali.

Sambamba na hayo, Meneja Mkapa amesema kuwa matarajio ya taasisi ni kwamba mafunzo waliopata wataenda kufanyia kazi na kupitia hayo shughuli za Mamlaka zitaimarika katika nyanja zote ambazo wanahusika kwa namna moja au nyingine.

Naye mdau wa kemikali, Naomi Sonyo, ameipongeza Mamlaka kwa kuendeleza semina za kila mwisho wa mwaka kwa sababu inawakumbusha na kuwajengea mbinu mpya za kukabiliana na kemikali hatarishi.







# HIFADHIDATA YA VINASABA YAZIDI KUPEWA KIPAUMBELE TANZANIA - Na Judith Meingarai

Wakati dunia ikiendelea kupiga hatua katika matumizi ya sayansi ya vinasaba, wataalam nchini wameelezea umuhimu wa uanzishwaji na ulinzi madhubuti wa hifadhidata ya Vinasaba (DNA) ili kulinda usalama wa taifa na faragha ya wananchi.

Akizungumza katika Kongamano la Siku ya Vinasaba Tanzania, lililofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Dodoma, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kairuki, Prof. Edda Vuhahula, alieleza kuwa hifadhi ya data ya Vinasaba ni nyenzo muhimu inayoweza kusaidia kutambua watu, kufuatilia magonjwa na hata kuunganisha ndugu waliopoteana.

Alisema kuwa endapo taarifa za Vinasaba vya mtu zitahifadhiwa, zinaweza kutumika baadaye kumtambua mtu aliyepata ajali, kufariki bila kutambulika, au hata kusaidia katika uchunguzi wa magonjwa ya kurithi.

"Ni muhimu sana nchi kuwa na hifadhidata ya DNA ya watu wake. Serikali tayari imeanza hatua hizo kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), na mchakato umefikia hatua nzuri," alisema Profesa Edda.

Hata hivyo, Profesa Edda alionya juu ya hatari inayoweza kujitokeza iwapo data za vinasaba zitaendelea kuchukuliwa na kupelekwa nje ya nchi bila udhibiti madhubuti. Alifafanua kuwa katika baadhi ya matukio, sampuli za wagonjwa hupelekwa nje ya nchi kwa uchunguzi, lakini hakuna uhakika wa nini kinafanyika kwa data hizo baada ya majibu kurejeshwa.

"Hatari yake ni kubwa. Mataifa ya nje yanaweza kupata uelewa wa kina wa Vinasaba vyetu, na hilo linaweza kutumika vibaya, hata kutengeneza madhara ya kiafya kwa vizazi vijavyo," aliongeza Profesa Edda.

Kwa mujibu wa mtaalam huyo, ingawa Tanzania ina sheria zinazodhibiti matumizi ya Vinasaba, bado kuna changamoto katika usimamizi wake. Alisisitiza kuwa taasisi zote zinazohusika na Vinasaba ikiwemo hospitali, vituo vya utafiti na vyombo vya dola zinapaswa kushirikiana na kufuata sheria kikamilifu.

Aidha, alisisitiza kuwa hakuna taasisi au mtu anayepaswa kufanya uchunguzi wa Vinasaba bila kibali cha serikali kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Pia, alishauri hatua kali zichukuliwe kwa wanaokiuka taratibu, ikiwa ni pamoja na kuchapisha tafiti bila idhini.

Kwa upande wa matumizi ya teknolojia ya DNA nchini, Profesa Edda alibainisha kuwa bado yako chini kutokana na uhaba wa maabara, wataalamu na uelewa mdogo wa wananchi.

Alipendekeza kuongezwa kwa maabara zenye viwango, kuimarisha mafunzo ya wataalamu, pamoja na kutoa elimu kwa umma ili wananchi watambue kuwa Vinasaba (DNA) ni sehemu ya utu wao na inapaswa kulindwa.

"Wananchi waelimishwe kuwa DNA ni utambulisho wao wa msingi. Si jambo la kuruhusu kila mtu kuifahamu au kuitumia bila mipaka," alisisitiza.

Naye Dkt. Irene Rweikiza, daktari wa binadamu anayesoma Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Bioteknolojia katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, alisema hifadhidata ya DNA ina umuhimu mkubwa katika kuimarisha huduma za afya nchini. "Kwa muda mrefu tumekuwa tukitumia zaidi taarifa za Vinasaba katika kutibu magonjwa, lakini mjadala wa mkutano huu umeonesha wazi umuhimu wa kuwa na kanzidata imara ya Vinasaba, hasa katika uchunguzi wa mapema wa magonjwa, ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kujitokeza baadaye," alisema Dkt. Irene.






Gcla Tanzania/gcla_official/gcla1895
gcla_tv/www.gcla.go.tz/0800116060 (Bure)



## MAMLAKA YAWAJENGEA UWEZO WATAALAM WA TIBA ASILI - Na Judith Meingarai

Serikali kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeendelea kuonesha dhamira ya kuinua sekta ya tiba asili nchini baada ya kuzindua mafunzo ya uchakataji salama wa dawa asili kwa wataalam wa tiba asili na tiba mbadala kutoka mikoa ya Mara, Simiyu na Mwanza.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo yaliyofanyika Machi 26, 2026 Ukerewe, Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Christopher Ngubiagai, alisema serikali inatambua mchango mkubwa wa wataalam wa tiba asili katika utoaji wa huduma za afya kwa Watanzania, huku akisisitiza kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Afya inayotambua rasmi tiba asili na tiba mbadala hapa nchini.

"Serikali imewaleta wataalamu wa GCLA ili kuhakikisha dawa za asili zinachakatwa kwa viwango vinavyokubalika, zinakuwa salama na zenye ubora unaoweza kushindana hata katika masoko ya kimataifa," alisema Ngubiagai.

Aidha, Ngubiagai Aliongeza kuwa jitihada hizo pia zinalenga kurasimisha sekta ya tiba asili na kuwajengea uwezo wataalam hao ili waweze kuwa sehemu ya mfumo rasmi wa huduma za afya nchini, hatua itakayoongeza heshima na uwajibikaji wao katika jamii, ambapo pia alihusisha mafunzo hayo na Dira ya maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050, akibainisha kuwa tiba asili ina mchango mkubwa katika kujenga Taifa lenye watu wenye afya bora, kukuza uchumi shindani unaotumia rasilimali za ndani pamoja na kuchochea ubunifu na ajira.

Katika hatua nyingine, Ngubiagai alisisitiza umuhimu wa kuzingatia misingi ya uchakataji salama ikiwemo usafi wa mazingira ya utayarishaji, matumizi ya vipimo sahihi vya dawa, ufungashaji bora pamoja na ushirikiano na wataalamu wa afya ili kuepuka madhara kwa watumiaji huku akiweka wazi kuwa tiba asili inaweza kuwa chanzo kikubwa cha mapato kupitia biashara na hata utalii wa tiba endapo ubora wake utaimarishwa na kuwekewa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Akimuwakilisha Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, Meneja wa Kanda ya Ziwa, John Wanjala, alisema kuwa lengo la Mamlaka ni kuhakikisha dawa zote zinazozalishwa zinakuwa salama, bora na zenye uwezo wa kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi huku akieleza kuwa mafunzo hayo yanalenga kuwasaidia wataalam wa tiba asili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, ikiwa ni pamoja na kuboresha uzalishaji na kupanua masoko ya bidhaa zao.

"Popote walipo wataalam wa tiba asili, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali tutaendelea kuwafikia kwa mafunzo na huduma za kitaalamu ili kuhakikisha wanatoa huduma zilizo bora na salama kwa jamii," alisema Wanjala.

Kwa upande wake Katibu wa chama cha Tiba Asili na Tiba Mbadala (TAMESOT), Maneke Malegeli, akizungumza kwa niaba ya washiriki, aliishukuru Mamlaka kwa mafunzo hayo kwa kuwa yamewasaidia kupata uelewa wa mbinu bora za utengenezaji, utayarishaji na ufungashaji wa dawa asili kwa kuzingatia viwango vinavyolinda afya za watumiaji na kuongeza kuwa mafunzo hayo pia yatawasaidia kujitofautisha na matapeli wanaotumia jina la tiba asili vibaya, huku pia akiiomba Mamlaka kuendelea kutoa elimu hiyo ili iweze kuwafikia wataalam wengi zaidi nchini.







# NPCC YAKUTANA NA WASIMAMIZI WA VIWANDA

Na Magreth Patrick

Kituo cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu (NPCC), imekutana na kuongea na Wakuu na Wasimamizi wa viwanda walivyovitembelea katika ziara yao iliyofanyika Novemba 11-14, 2025 katika wiki ya kuzuia sumu ya madini ya risasi duniani, lengo kuu likiwa ni kuleta usalama katika afya za watu na mazingira kwa ujumla.

Hayo yameelezwa Desemba 2, 2025 na Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira, Dkt. Peter Shimo, wakati akizungumza na Wakuu pamoja na Wasimamizi wa viwanda hivyo katika ukumbi wa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), jijini Dar es Salaam. Huku akiwasihi kuwa makini katika uzalishaji viwandani kwa kufuata kanuni na sheria zilizowekwa ili kuleta usalama wa wafanyakazi viwandani na pia katika mazingira kwa ujumla na mwisho kufanikisha suala zima la kudhibiti matukio ya sumu, hasa katika kuzuia sumu ya madini ya risasi.

"Ziara hiyo ilikuwa imepangwa ili kutoa elimu kwa jamii na kuipa uelewa jamii kwa ujumla juu ya Madhara yanayoletwa na sumu ya madini ya risasi ili kuweza kuokoa maisha ya watu na mazingira, kwasababu katika uchakataji wa betri katika viwanda vyetu kuna uwezekano mkubwa kuwepo kwa madini haya ya risasi" alisema Dkt. Shimo.

Aidha, amewasihi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali pindi wanapokumbana na changamoto yoyote katika viwanda vyao ili kuendelea kulinda afya za Wanajamii na Mazingira.

Kwa upande mwingine, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaalam ya Kudhibiti Matukio ya Sumu ya GCLA, Prof. Amos Mwakigonja, amewataka Wakuu na Wasimamizi wa viwanda hivyo wahakikishe Wafanyakazi wao katika viwanda wanapata vifaa maalum vya kujikinga na wakati wa uchakataji ili kuepusha madhara kwa afya zao. Vifaa hivyo ni pamoja na kuwapa viatu maalumu vya viwandani, mavazi na pia barakoa lengo kuu likiwa ni kuepusha madhara ya sumu ya madini ya risasi.

Prof. Amos Mwakigonja, alibaini kuwa Wafanyakazi wa viwanda hivyo hawapo salama kwa sababu ya kukosa vifaa maalum vya kujikinga wakati wa uchakataji pindi wanapofanya kazi, hali inayopelekea uwezeakano mkubwa wa kupata madhara yanayosababishwa na sumu ya madini ya risasi.

Kwa upande wake muwakilishi kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Jane Marwa, ametoa ushauri kwa Wakuu na Wasimamizi hao wa viwanda kuwa wanapaswa kuhakikisha usalama zaidi katika kuwalinda Wafanyakazi wao wa viwandani ili kuepusha madhara yanayosababishwa na sumu ya madini ya risasi. Amewashauri wao ndio wakawe mfano wa kuigwa kwa Wafanyakazi wao ili kutekeleza agizo la Serikali katika suala zima la kuhakikisha uasalama mahali pa kazi kwa Wafanyakazi hao.

Kwa upande wao Wakuu na Wasimamizi wa viwanda hivyo, wameweza kuishukuru Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kupitia kituo cha Taifa cha Taifa cha Kudhibiti Matukio ya Sumu (NPCC), kwa kuweza kuendelea kutoa elimu kuhusiana na madhara ya sumu ya madini ya risasi kwa kufanikisha kuweza kutembelea Viwanda vyao na kuwapa uelewa wa madini hayo sambamba na athari za madini hayo. Hivyo wameahidi kwenda kutekeleza yale waliyoyapokea kwenye kikao hicho.








# GCLA YAPONGEZWA KWA KUTOA HUDUMA BORA

Na Mwanaheri Jazza

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Camillius Wambura, ameipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kufanya kazi nzuri kupitia uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara wa makosa ya jinai unaofanywa na Mamlaka Hiyo.

IGP Wambura aliyasema hayo Leo Julai 6, 2025 wakati alipotembelea Banda la Mamlaka katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yanayofanyika jijini Dar es Salaam.

"Maabara yenu inatusaidia sana niwapongeze, Unajua sasa Hivi kila uhalifu ili kuutolea hukumu unahitaji uchunguzi wa kisayansi, sasa hivi mambo ya ajabu ajabu hayapo tena kwa sababu kuna sayansi ambazo zinaangukia kwenye Maabara zenu, hivyo Maabara yenu inatusaidia sana katika mambo haya". Alisema IGP Wambura.

Pia, IGP aliongeza kuwa ushirikiano wa karibu na Jeshi la Polisi pamoja na taasisi nyingine za haki na usalama ni muhimu katika kuhakikisha ushahidi wa kisayansi unatumika ipasavyo katika hatua zote za uchunguzi na uendeshaji wa mashauri.

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inashiriki Maonesho ya Sabasaba kwa kutoa elimu kwa wadau na wananchi kuhusu majukumu yanayofanywa na Mamlaka hiyo kwa umma.

Maonesho ya 49 ya Sabasaba kwa mwaka 2025 yanafanyika katika viwanja vya Maonesho vya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam yenye kauli mbiu ya *Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba Fahari ya Tanzania* yalianza rasmi Juni 28, 2025 na yanatarajiwa kuhitimishwa Julai 13, 2025.







# GCLA YAWAITA WAKULIMA KUFAHAMU UBORA WA MAZAO - Na Mwanaheri Jazza

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imewataka wadau mbalimbali wanaojishughulisha na kilimo kutembelea banda la Mamlaka ili waweze kupata elimu ya ubora wa mazao kabla ya kuingia sokoni kwa kuzingatia afya za walaji lakini pia na kujiimarisha kiuchumi.

Hayo yalisemwa Agosti 8, 2025 na Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kati, Dodoma, Magdalena Mtenga, katika Maonesho ya Wakulima Nanenane ambayo kitaifa yamefanyika katika Viwanja vya Nzuguni mkoani Dodoma.

"Nichukue fursa hii kuwaita wadau mbalimbali wanaojishughulisha na kilimo kutembelea banda la Mamlaka kujifunza majukumu na kazi mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka hii ambayo imepewa dhamana na Serikali ya kuwahudumia wananchi kupitia masuala ya kijamii, Afya pia na masuala ya jinai kwa kuwa tunashughulika pia na uchunguzi wa jinai.

Pia, waje tuweze kuwapatia elimu ambayo itawasaidia kufahamu ubora wa mazao kwa namna gani yanatakiwa yawe na ubora wa kitaifa na kimataifa kabla ya kuyapeleka sokoni, hii itasawasaidia pia kujiimarisha kiuchumi lakini na kuhakikisha Afya na usalama wa walaji uko salama". alisema Meneja Mtenga.

Akizungumzia lengo la Mamlaka kushiriki maonesho hayo, Meneja Mtenga alisema ni kujumuika pamoja na wadau na wananchi kwa ujumla kuwapa elimu kuhusu majukumu mbalimbali yanayofanyika katika Mamlaka ili yaweze kuwasaidia katika shughuli zao za kila siku, lakini pia kwa kuwa Mamlaka imepewa jukumu la kutoa elimu kwa wadau, wananchi na jamii, kuangalia ubora wa mazao na bidhaa mbalimbali za viwandani na majumbani lakini pia hata kwa wafanyabiashara kuwa na uhakika wa ubora wa bidhaa zao zinazoingia sokoni.

Kwa upande wake Patric Maliyabwana ambaye ni Mkurugenzi kutoka kampuni ya Patric Decoration, ameipongeza Mamlaka kwa jitihada za kuhakikisha inawafikia wadau wengi na kuwapatia elimu kuhusu majukumu inayotekeleza, pia amewashauri wadau mbalimbali kutembelea banda la Mamlaka na Ofisi zake ili waweze kupata maelezo na kujifunza zaidi.

"Nina furaha kubwa na nina shukuru sana kwa maswali ambayo nimeuliza hapa na jinsi nilivyojibiwa, nikiri kwamba kuna vitu nilikuwa sivifahamu lakini kupitia maonesho haya ya Nanenane nimefahamu majukumu makubwa ya taasisi hii ikiwemo masuala ya uhalali wa mtoto kwa mzazi. Niwashauri wadau mbalimbali waje kwenye banda hili watajifunza na kufahamu mambo mengi sio tu kwenye kilimo lakini hata katika maswala ya Afya na ujasiliamali," alisema Maliyabwana.

Maonesho ya 32 ya Wakulima Nanenane kwa mwaka 2025 yalibebwa na kauli mbiu ya "Chagua Viongozi Bora kwa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi."



*Mtumishi wa Mamlaka, Zabibu Duru (Kulia), akielezea majukumu mbalimbali ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mwananchi alietembelea banda la Mamlaka katika maonesho ya Nanenane ambayo Kitaifa yanafanyika katika Viwanja vya Nzuguni mkoani Dodoma, Agosti 1, 2025.*



# WATUMISHI WAASWA KUZINGATIA MTINDO BORA WA MAISHA - Na Regina Mwasolwa

Watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wameshauriwa kuzingatia mtindo bora wa Maisha sambamba na kufanya mazoezi ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza pamoja na msongo wa Mawazo wawapo kazini au nyumbani.

Ushauri huo umetolewa na Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt Fidelice Mafumiko, wakati akifungua mafunzo kuhusu afya ya akili, mapambano dhidi ya VVU na magonjwa yasiyoambukiza yaliyofanyika katika ukumbi wa Dkt. Mafumiko Dodoma Januari 28, 2026.

“Mafunzo haya yana lengo la kulinda afya za watumishi wa Mamlaka yetu ambayo yanahusisha kuzingatia mbinu bora za kujikinga na kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi na kwa upande mwingine mafunzo haya ni mhimu kwa sababu tunaamini elimu ya afya ya akili ni nguzo muhimu sana ya afya na maisha ya binadamu hivyo ni budi kuzingatia yote mtayoelekezwa katika mafunzo,” alisema Dkt. Mafumiko.

Kwa upande wake Daktari bingwa wa figo kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili ambae ni Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Dkt. Garvin Kweka, amesema lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwasaidia watumishi kuelewa na kutambua madhara ya tabia mbalimbali katika maisha ya kila siku na namna zinavyoathiri mazingira ya kazi na maisha ya familia.

“Nia yetu njema ni kuhakikisha watumishi wanaelewa na wanatambua madhara ya tabia inavyoweza kuathiri eneo la kazi, kwa hiyo tumegusia maeneo mengi ya tabia ya namna gani wale, namna gani wanywe na wawe na kiasi katika matumizi ya chumvi na sukari” alisema Dkt. Kweka.

Nao baadhi ya watumishi waliohudhuria mafunzo hayo wameishukuru Mamlaka kwa kuwapatia mafunzo hayo kwani yamewajenga na yamewafanya kuweza kujua umuhimu wa afya zao na kuepuka mambo yatakayoathiri afya zao na kikubwa zaidi kuwa imara na makini katika utendaji kazi wao wa kila siku.







## SIKU YA VINASABA YATIKISA, WADAU WAJADILI VIFAA TIBA - Na Mwanahija Masali

Wadau wa sekta ya afya, utafiti na sayansi ya Vinasaba wametumia maadhimisho ya siku ya Vinasaba kujadili umuhimu wa uuzaji na usambazaji sahihi wa vifaa tiba na vitendanishi huku wakisema kuwa ni msingi muhimu katika kuimarisha huduma za afya na maendeleo ya tafiti za kisasa Nchini.

Akizungumza Katika Maadhimisho hayo yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali (GCLA) yaliyofanyika tarehe 23 na 24 Aprili, 2026, katika Ukumbi wa Jakaya kiwete Jijini Dodoma, Joseph Masanja, kutoka taasisi ya usambazaji wa vifaa tiba ya Encore Medics alisema kuwa ubora wa vifaa tiba ni nguzo muhimu katika mafanikio ya tafiti na huduma za afya kwani itaweza kuwajengea hali ya kujiamini wafanyaji utafiti wakati wakiwa katika maabara zao.

Mdau kutoka taasisi inayohusika na Uuzaji na usambazji wa vifaa tiba Nchini (Pyramid Pharma limited), Eliud Burchad, anaamini kuwa mawazo yake ambayo amewasilisha katika siku hiyo ya maadhimisho ya siku ya vinasaba yataleta mabadiliko chanya katika upande wa vifaa vinavyotumika kufanyia uchunguzi wa Vinasaba vya Binadamu na mimea huku akiamini kuwa teknolojia hiyo italeta ubora wa ushindani wa matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kufanya uchunguzi.

“Uuzaji na usambazaji wa vifaaa tiba vyenye viwango ni muhimu katika kuimarisha uchunguzi wa kisayansi, nikiwa miongoni mwa wataalamu kutoka katika ofisi ya usambazaji wa vifaa vya kufanyia uchunguzi tumefanya tafiti nyingi ili kuona ni namna gani tunaweza kuwa na teknolojia ya kisasa katika kuboresha uhifadhi na namna ya uchukuaji wa sampuli mbalimbali, tukapata wazo la matumizi ya teknolojia ya kisasa ambayo inatumiwa na baadhi ya nchi mfano Afrika Kusini ambayo itatusaidia sana katika kuboresha uhifadhi wa Vinasaba,” alisema Eliud.

Aidha, Eliud aliongeza kwa kusema kuwa matumizi ya teknolojia za kisasa katika uchunguzi wa Maabara na Vinasaba yanaendelea kuboresha sekta ya afya huku akisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya taasisi za utafiti ,sekta binafsi na vijana katika kukuza ubunifu wa kisayansi.

## TAASISI ZIFANYIE KAZI MAAZIMIO YA SIKU YA VINASABA - Na Oscar Nkembo

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Christopher Kadio, amezitaka Taasisi kuhakikisha zinafanyia kazi maazimio ya Kongamano la Siku ya Vinasaba nchini Tanzania ili kufungua fursa kwa jamii kupitia teknolojia ya uchunguzi wa Vinasaba.

Mwenyekiti Kadio amesema hayo Aprili 24, 2026 wakati akihitimisha Kongamano la Siku ya Vinasaba nchini lililofanyika katika Kituo cha Mikutano Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

“Teknolojia ya Vinasaba inaweza kufanya kazi katika sekta mbalimbali kwa ajili ya maendeleo endelevu, Kongamano hili limetengeneza maazimio ambayo ni mwanzo mzuri wa mustakabali wa jambo hili, maazimio haya yafanyiwe uchambuzi wa kina na yanayoweza kutatuliwa na taasisi zetu yatatuliwe mara moja na yale yanapaswa kwenda ndazi za juu Bodi itafanya hivyo” alisema Kadio.

Bwana Kadio ameongeza kuwa kupitia Kongamano hili Wataalamu wameweza kujibu msingi wa maelekezo na matarajio ya viongozi wetu lengo kuu likiwa ni kwa namna gani teknolojia ya vinasaba inaweza kutoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya nchi yetu.

Khamis Said na Makame Khamis ni Watumishi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar, walisema Tanzania ina nafasi kubwa ya kupiga hatua katika Sayansi ya Vinasaba.

“Tanzania DNA Day Summit ina nafasi kubwa ya kuisaidia nchi yetu kupiga hatua kubwa katika maendeleo ya Sayansi ya Vinasaba na tunayo fursa kubwa ya kuweza kuisaidia jamii kutatua changamoto mbalimbali kupitia Vinasaba, kwa hiyo tumepata Dira ya muelekeo wa nchi katika Sayansi hii” alisema.



**Christopher Kadio**
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali





# MAAFISA WA POLISI WAPEWA MAFUNZO YA USIMAMIZI WA SAMPULI ZA JINAI - Na Judith Meingarai

Wataalamu kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) wametoa mafunzo kwa askari wa Jeshi la Polisi kuhusu usimamizi wa sampuli za makosa ya jinai, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha matumizi ya sayansi katika upelelezi na utoaji wa ushahidi mahakamani.

Mafunzo hayo yaliyofanyika katika Chuo cha Taaluma ya Polisi, Dar es Salaam Machi 12, 2026, yamelenga kuwajengea uwezo askari katika ukusanyaji, utunzaji na usafirishaji sahihi wa sampuli za jinai kutoka eneo la tukio hadi maabara kwa ajili ya uchunguzi wa kisayansi.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), Dkt. Lazaro Mambosasa, alisema ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni muhimu katika kuhakikisha ushahidi wa kisayansi unatumika ipasavyo katika upelelezi wa makosa ya jinai.

"Moja ya majukumu makubwa ya Jeshi la Polisi ni kufanya upelelezi wa makosa ya jinai. Katika mchakato huo tunashirikiana na taasisi mbalimbali, ikiwemo Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ambayo ina jukumu muhimu la kuchambua sampuli na kutoa majibu ya kisayansi yanayotumika kama ushahidi mahakamani," alisema Dkt. Mambosasa.

Alifafanua kuwa sampuli zinazokusanywa kutoka katika maeneo ya matukio ya uhalifu ni miongoni mwa nyenzo muhimu zinazotumika kuthibitisha makosa ya jinai mahakamani, kwani husaidia kumuunganisha mtuhumiwa na tukio lililotendeka kupitia ushahidi wa kisayansi.

"Unapozungumzia sampuli, unazungumzia moja ya nyenzo muhimu za ushahidi. Hizi ndizo zinazosaidia kuthibitisha kosa mahakamani ili pale ambapo mtuhumiwa anapatikana na hatia, ahukumiwe kwa mujibu wa sheria," alieleza.

Dkt. Mambosasa alisisitiza kuwa uchunguzi wa kisayansi una nafasi kubwa katika mfumo wa kisasa wa upelelezi wa makosa ya jinai, akibainisha kwamba kesi isiyofanyiwa uchunguzi wa kisayansi ipasavyo inaweza kuondolewa mahakamani kwa kukosa ushahidi wa kumuunganisha mtuhumiwa na kosa linalodaiwa kutendeka. Ndiyo maana mafunzo haya yanayotolewa na wataalamu wa GCLA ni muhimu sana kwa askari wa jeshi la Polisi.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa mafunzo hayo, Isaya Mayagila aliwashukuru wataalamu wa GCLA kwa kuwapatia mafunzo yaliyowaongezea uelewa kuhusu usimamizi wa sampuli za ushahidi katika uchunguzi wa makosa ya jinai.

"Mafunzo haya yametupatia maarifa muhimu kuhusu namna sahihi ya kukusanya, kuhifadhi na kusafirisha sampuli za ushahidi. Tutaenda kuyatumia kikamilifu katika maeneo yetu ya kazi ili kuongeza ufanisi wa upelelezi," alisema.

Wakati huo huo, wananchi wametakiwa kushirikiana na vyombo vya dola kuepuka kuingilia eneo la tukio la uhalifu, hatua ambayo inaweza kusababisha kupotea au kuvurugika kwa ushahidi muhimu.

Mafunzo hayo ni sehemu ya juhudi za kuimarisha ushirikiano kati ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Jeshi la Polisi katika matumizi ya sayansi ya uchunguzi wa jinai ili kusaidia upatikanaji wa ushahidi na kuhakikisha haki inatendeka kwa mujibu wa sheria.





# WASIMAMIZI NA WACHUNGUZI WA MAABARA WATAKIWA KUPATA MAFUNZO KABLA YA KUSAJILIWA - Na Okello Thomas

Wasimamizi na Wachunguzi wa Maabara za Vinasaba vya Binadamu wametakiwa kupata mafunzo kuhusu Taratibu, Kanuni na Sheria zote zinazohusiana na Udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu kabla ya kusajiliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambae ndiye msimamizi wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Sehemu ya Usajili na Ukaguzi wa Maabara ya Vinasaba na Sayansi Jinai, Fidelis Segumba katika mafunzo ya kujenga uelewa wa masuala yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu kwa wadau yaliyofanyika katika ukumbi wa Mkemia, jijini Dar es Salaam Agosti 19, 2025.

“Lengo la Sheria hii ni kulinda taarifa za Vinasaba zinazozalishwa kutokana na uchunguzi unaofanyika kupitia Teknolojia ya Vinasaba. Hivyo, kwa mujibu wa Sheria hii wadau wote wanaohusika na matumizi ya Teknolojia ya Vinasaba vya Binadamu ikiwemo kufanya uchunguzi wa kimaabara, tafiti au namna nyingine yoyote ile, mnapaswa kusajiliwa na Mkemia Mkuu wa Serikali. Kabla ya Usajili, wadau wote mnatakiwa kupata mafunzo maalumu ya kuhusiana na matakwa ya Sheria na Kanuni zake, pamoja na uendeshaji wa Maabara za vinasaba vya binadamu,” alisema Segumba.

Naye, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Advera Ngaiza, ameipongeza Mamlaka kwa utoaji wa elimu kwa wadau hao kwani wameweza kutambua miongozo ya kudhibiti na kuenenda katika habari ya vinasaba vya binadamu.

“Mafunzo haya ni muhimu kwa sababu hatukuwa tunafahamu Sheria za Udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu hasa taarifa ambazo muhimu sana tukidhani kama taarifa nyingine zozote, lakini kumbe Vinasaba vya Binadamu ni zaidi ya zile taarifa za mgonjwa kwa sababu kama isipodhibitiwa inaweza ikatumika ndivyo sivyo na pia ikaleta madhara kwa mtu binafsi au kwa taifa kwa ujumla,” alisema Daktari Ngaiza.







# MAABARA YA SAYANSI JINAI KEMIA YAPATA ITHIBATI - Na Sylvester Omary

Maabara ya Sayansi Jinai Kemia ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imefanikiwa kupata ithibati ya kimataifa ya uchunguzi wa kimaabara kutoka Taasisi ya Ithibati ya Jumuiya ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADCAS).

Akiongea jijini Dar es Salaam Aprili 10, 2026 baada ya kupokea cheti cha ithibati hiyo kutoka SADCAS, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amewapongeza watumishi wote wa Mamlaka kwa kufanikisha kupatikana kwa ithibati hiyo na kuwataka watumishi kuendelea kuzingatia misingi ya utendaji kazi kulingana na matakwa ya ithibati ili kuendelea kuzilinda.

"Nawapongeza watumishi wa Mamlaka kwa mafanikio makubwa ya kuwezesha kuipata ithibati ya maabara ya sayansi jinai Kemia ambayo sasa imekamilisha idadi ya maabara zetu zote saba kuwa na ithibati. Ni kazi kubwa imefanyika kufikia hatua hii na sasa tunapaswa kuendelea kufanyakazi kwa bidii na weledi ili kuendelea kuzilinda ithibati hizi kulingana na matakwa ya SADCAS pamoja na faidi kwa Mamlaka yetu" alisema Dkt. Mafumiko.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai, David Elias, amesema anaishukuru Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na watumishi wa Mamlaka kwa kuweza kufanyakazi kwa juhudi na bidi na kufanikisha lengo la Mamlaka kuwezesha maabara zote saba kupata ithibati za kimataifa katika masuala ya uchunguzi wa kimaabara.

"Kwa kweli hii ni hatua ya kujivunia sana kwa Mamlaka, napenda kutoa shukrani kwa kila mmoja kuanzia Bodi, Menejimenti na watumishi kwa sababu kwa umoja wetu na juhudi tumeweza kutimiza lengo hili la kuwa na ithibati katika maabara zetu zote. Hii inatuongezea sifa na hadhi zaidi katika utekelezaji wetu wa majukumu ya kiuchunguzi wa kimaabara kitaifa na kimataifa. Hatua hii iwe chachu kwetu ya kuendelea kufanyakazi kwa weledi na juhudi zaidi ili kulinda hizi ithibati pamoja na sifa ya Mamlaka" alisema Mkurugenzi Elias.

Upatikanaji wa ithibati kwa Maabara ya Sayansi Jinai Kemia kunafanya jumla ya maabara zote saba za Mamlaka kuwa na ithibati ya kimataifa kutoka SADCAS. Maabara nyingine ambazo zina ithibati ni Maabara ya Sayansi Jinai Baiolojia na Vinasaba, Maabara ya Sayansi Jinai Toksikolojia, Maabara ya Maikrobailojia, Maabara ya Mazingira, Maabara ya Chakula na Dawa na Maabara ya Ofisi ya Kanda ya Ziwa iliyopo Mwanza.



*Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko (kulia) akimkabidhi Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira, Dkt. Shimo Peter (kushoto) vyeti vya ithibati vilivyohuishwa vya maabara tatu za Mazingira, Mikrobaiolojia na Chakula na Dawa baada ya kupokea vyeti hivyo kutoka SADCAS. Tukio hilo limefanyika kwenye Ofisi za Mamlaka jijini Dar es Salaam, Aprili 10, 2026.*



# GCLA YASISITIZA UDHIBITI WA KEMIKALI HATARISHI

Na Judith Meingarai





Serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa usimamizi madhubuti wa kemikali za viwandani na majumbani ili kulinda afya za wananchi na mazingira dhidi ya matumizi mabaya ya kemikali hatarishi.

Akifungua Mkutano wa Mwaka wa Wakaguzi wa Kemikali na Maabara za kemia uliofanyika katika Hoteli ya Corridor Springs Arusha, Juni 6, 2026, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, alisema kuwa kupitia Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Serikali imeikabidhi Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali jukumu la kusimamia mnyororo mzima wa kemikali pamoja na kemikali bashirifu zinazoweza kutumika kinyume na matumizi stahiki ya kemikali hizo.

Alisema wakaguzi ndio nguzo muhimu katika kuhakikisha kemikali hizo zinadhibitiwa ipasavyo kupitia ukaguzi, usajili, uchukuaji wa sampuli na ukaguzi wa maabara.

“Wakaguzi ndio mliopo mstari wa mbele katika kulinda afya ya jamii, mazingira na wananchi kwa ujumla dhidi ya matumizi yasiyo sahihi ya kemikali hatarishi,” alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma kwa kujiepusha na rushwa, lugha zisizofaa kwa wadau na ucheleweshaji wa huduma.
Kwa upande wake, mwakilishi wa wakaguzi wa kemikali, Melk Mgonga, aliwahimiza wakaguzi kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa bidii, uadilifu na kuzingatia sheria ili kuhakikisha maazimio yote yatakayofikiwa katika mkutano huo yanatekelezwa kikamilifu.

"Twendeni tukatekeleze majukumu yetu kwa weledi na uzalendo, tuimarishe shughuli za ukaguzi kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa, na tuhakikishe kuwa maazimio yote yatakayopitishwa katika mkutano huu yanatekelezwa kwa ufanisi kwa manufaa ya taasisi na Taifa kwa ujumla," alisema Mgonga.

Mkutano huo wa siku mbili unatarajiwa kujadili mikakati ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ya ukaguzi na usajili wa kemikali pamoja na maabara za kemia nchini.



# MAAFISA WAANDAMIZI WATAKIWA KUWA NA MTAZAMO CHANYA

Na Sylvester Omary

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amewataka Maafisa Waandamizi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuwa na mtazamo chanya na kuwaongoza watumishi wengine katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi.

Mkemia Mkuu wa Serikali aliyasema hayo Aprili 10, 2026, jijini Dar es Salaam wakati akifungua mafunzo ya Usimamizi na Maadili ya Uongozi kwa Maafisa Waandamizi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

"Sisi ni viongozi kulingana na ngazi tulizonazo za kiutumishi na tunapaswa kutambua wajibu wetu wa kuongoza watumishi wenzetu kwenye Kurugenzi, Ofisi za Kanda, Vitengo na kwenye Maabara kwa sababu ni wajibu wetu wa msingi. Tunapaswa kukubali mabadiliko na kuwa na mtazamo chanya juu ya majukumu ya taasisi tunayotekeleza.

Kuchangamana na kufanyakazi pamoja ni jambo la msingi kwa sababu tunapaswa kujua Mamlaka itabadilishwa na sisi tuliopo ndani na kufikiria namna ya kuishi vizuri kama familia moja. Lazima tuijenge taasisi yetu na kwa kupitia kundi hili la watumishi naamini litaleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji" alimaliza Dkt. Mafumiko.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Evaclotida Kapinga, akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Maafisa hao, alisema anamshukuru Mkemia Mkuu wa nasaha zake na kuwataka washiriki wa mafunzo kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Mkemia Mkuu wa Serikali hasa katika kuwalea watumishi wengine.

"Tunapaswa kuwalea na kuwasapoti watumishi wa chini yetu ili nasaha na maelekezo yaliyotolewa na Mkemia Mkuu wa Serikali kuweza kuyafikia. Bila kuwashika mkono na kuwavuta hawataweza kufikia hapa tulipofikia sisi. Tusiwaache nyuma pamoja na changamoto zao tunatakiwa kwenda nao kwa sababu taasisi inaishi" alimaliza Mkurugenzi Evaclotida.



*Kundi la Maafisa Waandamizi wakifanya zoezi kwa vitendo kama njia ya kujifunza namna ya kufanya kazi kwenye mazingira na watu tofauti wakati wa mafunzo ya usimamizi na maadili ya uongozi yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Februari 12, 2026.*



# WAKAGUZI WAASWA KUFANYA MAAMUZI KWA KUZINGATIA MAARIFA NA UJUZI - Na Okello Thomas

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, amewataka wakaguzi wapya Kemikali na Maabara za Kemia kutambua wajibu na mamlaka watakayokuwa nayo kwa mujibu wa matakwa ya sheria na kufanya maamuzi kwa kuzingatia maarifa na ujuzi kwenye majukumu yao.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, alisema hayo Novemba 10, 2025 wakati akifungua mafunzo kwa Wakaguzi wapya (39) wa Kemikali na Maabara za Kemia yaliyofanyika katika Ofisi za Kanda ya Mashariki, Dar es Salaam.

"Nawaelekeza mtumie nafasi hii adhimu kuwa wasikivu na wenye utayari wa kujifunza kwa kusikiliza watoa mada na kuuliza maswali kwa lengo la kujenga uelewa zaidi. Kwa kuzingatia maarifa na ujuzi mtakaopata katika mafunzo haya, ni matumaini yangu kuwa mtajenga uelewa na weledi wa kutosha kutekeleza jukumu hili muhimu kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali," alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, Mkemia Mkuu wa Serikali alisisitiza wakaguzi kuepuka kuwa na changamoto zinazotokana na kukosekana weledi wa mkaguzi hasa katika kujaza dodoso kwa makini wakati wa ukaguzi na kuandika taarifa sahihi na stahiki.

Pia, Dkt. Mafumiko ameongeza kuwa ni takwa la kisheria kwa wakaguzi kupata mafunzo hayo kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kupewa vitambulisho kwa ajili ya kufanya ukaguzi kwa wadau wanaojishughulisha na kemikali au uchunguzi katika Maabara za Kemia.

mafunzo hayo kabla ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kupewa vitambulisho kwa ajili ya kufanya ukaguzi kwa wadau wanaojishughulisha na kemikali au uchunguzi katika Maabara za Kemia.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo alisema kuwa mafunzo hayo yameandaliwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakaguzi wapya pamoja na kukidhi matakwa ya kisheria, na hivyo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kwa mujibu wa Sheria.



*Watumishi wa Mamlaka wakifuatilia mada mbalimbali katika siku ya kwanza ya Mafunzo kwa Wakaguzi wapya wa Kemikali na Maabara za Kemia yaliyofanyika katika Ofisi za Kanda ya Mashariki zilizopo kwenye jengo la Ushirika, Dar es Salaam, Novemba 10, 2025.*



Gcla Tanzania/gcla_official/gcla1895
gcla_tv/www.gcla.go.tz/0800116060 (Bure)













Document Control

















TUGHE
TUGHE
TUGHE
TUGHE
TUGHE






Kifungu cha
15 na 15A

















# KANDA YA KATI YAIMARISHA USIMAMIZI WA MAABARA ZA KEMIA - Na Mwanahija Masali

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Daniel Ndiyo, amewataka wadau wa kemikali wa Kanda ya Kati kufanya usajili wa Maabara za Kemia ili kuepusha uchepushaji wa kemikali katika utengenezaji wa dawa.

Mkurugenzi Ndiyo alisema hayo Machi 3, 2026, jijini Dodoma wakati akifungua Mafunzo ya Udhibiti na Usimamizi wa Maabara za Kemia kwa wadau wa kemikali kutoka Kanda ya Kati yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Kanda ya Kati.

"Kitu cha kwanza ambacho naweza kuzungumzia kwenu wadau inabidi tujitahidi sana kuzifanya kazi zetu kuwa rasmi kwa kufanya usajili wa hizi maabara na bidhaa zetu za kemikali, kwa sababu uhifadhi wa kemikali unahitaji umakini wa hali ya juu na pia wataalamu ambao watakusaidia kukupatia maelekezo ya namna gani unatakiwa kuhifadhi kemikali kwa uangalifu, Pia, itasaidia kupunguza uwepo wa kemikali hatarishi kwa jamii" alisema Daniel Ndiyo.

Naye Meneja wa Mamlaka, Ofisi ya Kanda ya Kati, Magdalena Mtenga, aliwashukuru wadau kwa kuweza kuhudhuria mafunzo hayo ambayo moja kwa moja yameweza kuzungumzia Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali na usimamizi wa Maabara za Kemia, huku akisema kuwa mafunzo hayo yatawajenga katika kufanya kazi za uzalishaji na utumiaji wa kemikali kwa usahihi katika maabara zao.

Maabara za Kemia, huku akisema kuwa mafunzo hayo yatawajenga katika kufanya kazi za uzalishaji na utumiaji wa kemikali kwa usahihi katika maabara zao.

"Tumeandaa mafunzo haya ili kuweza kukutana na wadau wa Maabara za Kemia pia inahusika na usimamizi wa maabara za kemia. Kwa kifupi imetupatia fursa ya kuwapa elimu namna gani wanaweza kusajili kemikali zao na namna wanatakiwa kufuata sheria ya kemikali na pia tumeweza kuchukua maoni yao kuhusu sheria ya kemikali na tutaenda kuyafanyia kazi" alisema Magdalena.



*Meneja wa Ofisi ya Kanda ya Kati, Magdalena Mtenga, akiwasilisha mada kuhusu Majukumu ya Mamlaka kwa Wadau wa Maabara za Kemia (hawapo pichani) katika Mafunzo ya Udhibiti na Usimamizi wa Maabara za Kemia yaliyofanyika Hoteli ya Zabibu, Dodoma Machi 31,2026.*





# GCLA YASISITIZA UBORA NA USALAMA WA DAWA ASILI

Na Judith Meingarai

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, imewataka waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala kuendelea kuboresha kazi zao na kuzalisha dawa salama na zenye ubora kwa kuwa hatua hiyo itasaidia katika kukuza soko la dawa asili nchini na kimataifa, sambamba na kuinua uchumi wa taifa.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Kanda ya Ziwa, Faustine Wanjala kwa niaba ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, katika mafunzo kwa waganga wa tiba asili na tiba mbadala yaliyolenga kuimarisha ubora, usalama na ufanisi wa dawa wanazozalisha, yaliyofanyika tarehe 23 hadi 24 Machi 2026, mkoani Geita.

"Ni muhimu kutumia elimu hii katika kuboresha utengenezaji wa dawa asili ili kuhakikisha zinakidhi viwango vya ubora na usalama unavyotakiwa. Hii itaziwezesha dawa hizo kuingia na kushindana katika masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema Wanjala.

Aidha, Wanjala aliwasisitiza waganga hao kutumia huduma za maabara za GCLA kwa ajili ya kupima ubora na usalama wa dawa wanazozalisha pamoja na kuzisajili ili ziweze kutambulika rasmi na kutumika katika vituo vya afya, zahanati, kliniki na hospitali.

Kwa upande wake, mwakilishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Tiba Asili, ambaye pia ni msemaji mkuu wa ofisi ya Katibu Mkuu wa Tiba Asili Taifa, Manike Maregeli, aliishukuru GCLA kwa kuwezesha mafunzo huku akisema kuwa mafunzo hayo ni mwanzo mzuri wa safari ya kuboresha taaluma ya tiba asili nchini.

"Naamini elimu tuliyoipata hapa itatusaidia kubadilika na kuacha mifumo ya zamani na badala yake kuzingatia uchakataji salama na wa kisasa wa dawa za asili," alisema Maregeli.

Naye mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Geita na Mratibu wa Tiba Asili na Tiba Mbadala mkoani humo, Cleophace Prosper, aliipongeza GCLA kwa kuandaa mafunzo hayo yenye tija kwa waganga wa kanda hiyo huku akiwataka washiriki kuhakikisha wanatekeleza maelekezo yote waliyopewa ili kuboresha huduma zao na kuongeza ushindani wa bidhaa zao sokoni.

Mafunzo hayo yamehudhuriwa na jumla ya waganga takribani 212 kutoka mikoa ya Geita, Kagera na Shinyanga, yakitoa fursa kwa washiriki kujifunza mbinu bora za uchakataji wa dawa asili, usafi, pamoja na matumizi sahihi ya vifungashio ili kufikia viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa huku yakitarajiwa kuwa hatua muhimu katika kuleta mapinduzi ya kisasa katika sekta ya tiba asili.



*Kaimu Meneja wa Maabara ya Chakula na Dawa, Everlight Matinga (kushoto) akimsikiliza mganga wa tiba asili na tiba mbadala, Jackline Mollel, akionesha namna ambavyo anafungasha bidhaa zake kabla ya kupeleka sokoni.*



# MAFUZO YA UCHUKUAJI SAMPULI YAWAIMARISHA WATUMISHI - Na Magdalena Mabula

Mkemia Mkuu wa Serikali Dkt. Fidelice Mafumiko, ameipongeza Kanda ya Mashariki kwa kuendelea kutoa elimu ya uchukuaji sahihi na salama wa sampuli mbalimbali kwa watumishi wa Kanda hiyo hatua itakayopelekea kurahisisha uchunguzi wa kimaabara.

Dkt. Mafumiko ameyasema hayo Januari 17-18, 2026 wakati akifungua mafunzo ya uchukuaji sahihi na salama wa sampuli za uchunguzi wa kimaabara kwa watumishi wa Kanda ya Mashariki yaliyofanyika Dar es Salaam.

"Nipende kuwapongeza sana kwa hatua mliyofikia ya uchukuaji na uhifadhi mzuri wa sampuli za kemikali kutoka kwa wateja ili kurahisisha uchunguzi wa kimaabara, kwa hiyo tuendelee kuilinda na kuiheshimu imani tuliyopewa na Serikali kwa kutambua kuwa Serikali imetuamini. Hivyo, tuhakikishe tunachukua sampuli kwa umakini na kuzihifadhi vizuri kwani ubora wa sampuli ndio ubora wa matokeo" alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, Dkt. Mafumiko amewataka watumishi hao kuwa karibu na Maabara za uchunguzi ili kuweza kujifunza namna mitambo mbalimbali inavyofanya kazi katika uchunguzi wa sampuli hizo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira, Dkt. Peter Shimo, amesisitiza kila mtumishi kuzingatia mwongozo wa uchukuaji sampuli kwani kufuata taratibu hizo kutasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi.

Naye, Meneja Ofisi ya Kanda ya Mashariki, Danstan Mkapa, amemshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, kwa kuweza kuwapatia mafunzo hayo kwani yatasaidia kuongeza uelewa na ujuzi kwa watumishi hao katika utekelezaji wa majukumu ya kiutafiti hasa katika uchukuaji na uhifadhi sahihi wa Sampuli.







# TANAPA YAIPONGEZA MAMLAKA KWA KUTOA RIPOTI KWA WAKATI - Na Oscar Nkembo

Mjumbe wa Menejimenti ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) amesema Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inatoa matokeo ya Uchunguzi kwa wakati na akasisitiza kuwa endapo TANAPA itaitumia vizuri maabara za uchunguzi za Mamlaka basi itafanikiwa.

Mjumbe huyo amesema hayo Februari 4, 2026 wakati Menejimenti ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) ilipotembelea Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Makao Makuu, Dodoma kwa lengo la kujifunza na kupata uzoefu wa namna Mamlaka inavyofanya Uchunguzi wa Sampuli za Wanyamapori.

"Mlango wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali uko wazi siku zote, nilikuwa Taasisi nyingine awali na sampuli zangu zote nilizowahi kuleta hapa hazijawahi kuchelewa na kesi zangu zote nilishinda. Kwa sasa niko TANAPA naamini mlango wa Mamlaka hii uko wazi tukiutumia tutafanikiwa sana" alisema mjumbe huyo.

Kwa upande wake Mjumbe wa Bodi ya TANAPA, Dkt. Robert Fyumagwa aliipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi na kutumia vifaa na teknolojia ya kisasa inayochochea utoaji wa matokeo ya uchunguzi kwa wakati.

"Tunawapongeza sana kwa kuendelea kufanya kazi nzuri inayosaidia katika utoaji wa ushahidi wa makosa ya Jinai kama ujangili wa wanyamapori" alisema Dkt. Fyumagwa.

kufanya kazi nzuri inayosaidia katika utoaji wa ushahidi wa makosa ya Jinai kama ujangili wa wanyamapori" alisema Dkt. Fyumagwa.

Naibu Kamishna wa Uhifadhi, Massana Mwishawa anaesimamia Uhifadhi na Maendeleo TANAPA, Makao Makuu, amesema ushirikiano baina ya Taasisi hizo mbili una tija kubwa kwenye maendeleo ya taifa.

"Tushirikiane ili kuzuia matukio yote ya ujangili ili wanyama wawe hai, misitu iwe hai, kwani uchumi wa taifa unategemea uhifadhi na utalii, tuko tayari kuhakikisha Sampuli zinafika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Mwaka 2025 mmechunguza sampuli 183 na kuzitolea ushahidi, ni sampuli chache sana ukilinganisha na zile tunazozikusanya na kuhitaji msaada, tutahakikisha zinafika hapa. Tumerithishwa tuwarithishe" alimaliza Naibu Kamishna Massana.

Akizungumza kwa niaba ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Daniel Ndiyo, ameishukuru Menejimenti ya TANAPA huku akiwakataka kuitumia Mamlaka kufanikisha utendaji wa kazi.

"Niwashukuru Sana, Mamlaka hii ni ya kwenu na iko tayari kwa ajili ya kushirikiana nanyi, itumieni vizuri ili kufanikisha kulinda maslahi ya Taifa na karibuni sana siku nyingine" alisema Ndiyo.



*Mtumishi wa Mamlaka, Mohamed Saidi (picha ya juu kushoto) akieleza mchakato wa uchunguzi wa Sampuli za Wanyamapori kwa Wajumbe wa Menejimenti ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) wakati walipotembelea Ofisi za Mamlaka, Makao Makuu Dodoma, Januari 4, 2026.*




# WASIMAMIZI WAPEWA MBINU ZA UDHIBITI SALAMA WA KEMIKALI - Na Okello Thomas

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeendelea kutoka mafunzo kwa wadau wanaojihusisha na biashara na matumizi ya kemikali kwa lengo la kuendelea kuwajengea uwezo wa usimamizi salama wa kemikali ili kulinda afya ya jamii na mazingira.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo katika hoteli ya Edema mkoani Morogoro Novemba 26, 2025, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko amesema kuwa mafunzo ya usimamizi salama wa kemikali yanakwenda sambamba na Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals – SDG) ambayo yanalenga kufikia maisha bora na endelevu kwa wote ifikapo mwaka 2030.

"Ili kufikia lengo juu ya afya njema na salama, suala la kuzuia au kupunguza madhara ya kemikali kwa afya na mazingira ni lazima lipewe kipaumbele na pia ili kufikia lengo juu ya maji salama na safi, ni lazima kuzuia au kupunguza utiririshaji wa kemikali na kemikali taka hatarishi kwenye vyanzo vya maji ili kulinda afya ya jamii na mazingira," alisema Dkt. Mafumiko.

Aidha, Mkemia Mkuu wa Serikali ameongeza kuwa hayo yote yatafikiwa tu endapo wahusika wakiwemo wasimamizi wa kemikali wanakuwa na elimu sahihi juu ya matumizi salama ya kemikali ambayo wataifuata katika maeneo yao ya kazi na kuhakikisha usalama katika jamii inayozunguka maeneo hayo.

Pia, Dkt. Mafumiko ameeleza kuwa kupitia mafunzo hayo, wasimamizi wa kemikali watajengewa uelewa wa namna ya kuzuia, wakati wa matumizi yake na hivyo kuwataka washiriki wa mafunzo kufikisha elimu watakayopata kwa makundi mengine kulingana na wigo wa majukumu wanayosimamia pamoja na watu walio chini yao katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya kemikali.

"Mtakuwa mabalozi wa kuwajengea uelewa wananchi wa kawaida walioko karibu na maeneo yenu ya kazi kwa kutambua kemikali husika pamoja na madhara yake, hatua za kujikinga na njia za kusaidia endapo litatokea tatizo," aliongezea Dkt. Mafumiko.

Naye, Kaimu Meneja Ofisi ya Kanda ya Kati, Fidelis Chrizant, amewapongeza wadau waliojitokeza kushiriki mafunzo hayo na kuahidi kuwapa elimu iliyo bora kuhusu masuala ya usimamizi salama wa kemikali na kuwataka wawe huru kuuliza maswali na kujenga hoja.



*Washiriki wa mafunzo ya usimamizi salama ya kemikali wakifuatilia mada mbalimbali zilizowasilishwa na wawezeshaji kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Ofisi ya Kanda ya Ziwa.*




# WANAWAKE WATAKIWA KUTUMIA FURSA KUJILETEA MAENDELEO - Mwanaheri Jazza na Rosemary Celu

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, amewataka wanawake nchini kuendelea kujituma katika kazi na kutumia fursa wanazopewa ili kuchangia maendeleo ya taifa pamoja na kujijengea ustawi wao binafsi.

Akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Mbande wilayani Kongwa Machi 8, 2026, Senyamule alisema wanawake wanapaswa kutumia ipasavyo fursa za usawa na uwezeshaji zinazotolewa na kuunga mkono waliofanikiwa kiuchumi na kijamii, pia kuwapongeza wakazi wa Mkoa wa Dodoma kwa hatua kubwa waliyoipiga katika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Napenda kuwataka kutumia siku hii kuhamasisha kuhusu fursa za haki za uchumi na kuwaunga mkono wanawake walioonesha njia, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wanaume na wanawake wote wa Mkoa wa Dodoma kwa jitihada wanazofanya katika kupambana na ukatili wa kijinsia. Mwaka 2024 tulikuwa na matukio 17,927 yaliyohusisha wanawake na wanaume, lakini kutokana na juhudi za Serikali na jamii, matukio hayo yamepungua hadi kufikia 8,020 mwaka 2025, sawa na punguzo la takribani asilimia 44.7," alisema Senyamule.

Kwa upande wao, baadhi ya wanawake kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) wamesema taasisi hiyo imekuwa mstari wa mbele katika kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika kazi na shughuli za maendeleo.

Happyness Ndegeiswa kutoka Makao Makuu ya Mamlaka jijini Dodoma alisema uwezeshaji unaotolewa na ofisi yao umewapa wanawake fursa ya kuonyesha uwezo wao katika utumishi wa umma.

"Katika kuadhimisha siku hii ya wanawake duniani, napenda kuipongeza Mamlaka kwa kutujali na kutuwezesha wanawake kushiriki maadhimisho haya kila mwaka. Pia kumekuwa na ongezeko la watumishi wanawake, jambo linaloonesha dhamira ya kuimarisha usawa wa kijinsia kazini," alisema Ndegeiswa.

Aliongeza kuwa wanawake wanapaswa kuendelea kujituma katika majukumu yao ili kuongeza pato la Taifa pamoja na kuhakikisha wanatimiza wajibu wao katika malezi ya watoto na ustawi wa familia.

Naye Asanath Ally kutoka Ofisi ya Kanda ya Kati alisema usawa wa kijinsia ni msingi muhimu wa maendeleo ya jamii na ni muhimu jamii kutambua kuwa haki na usawa wa wanawake sio suala lao peke yao bali ni msingi wa maendeleo ya jamii nzima, kwani mwanamke akiwezeshwa ana uwezo mkubwa wa kuchangia maendeleo ya familia na taifa.

Kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani huadhimishwa kila mwaka Machi 8, ambapo mwaka huu wa 2026 yalibeba kaulimbiu isemayo:
**"Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050."**




*Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule, akizungumza wakati wa hafla ya Siku ya Wanawake Duniani katika viwanja vya Mbande wilayani Kongwa Machi 8, 2026.*



# WANAWAKE GCLA WATOA MSAADA KWA WATOTO NJITI

Na Okello Thomas

Katika kuhitimisha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2026, wanawake wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wametoa misaada kwa watoto njiti katika hospitali ya Taifa Muhimbili.

Akizungumza kwa niaba ya wanawake wa Mamlaka, Mwenyekiti wa Wanawake GCLA, Veronica Chiligati alisema wametoa msaada huo wa mahitaji mbambali kwa lengo la kuwasaidia watoto njiti waliozaliwa katika hospitali ya Taifa Muhimbili iliyopo jijini Dar es Salaam, Machi 6, 2026.

"Kama ilivyo utamaduni wetu wa kurudisha kwa jamii, katika kila mwaka kuelekea Siku ya Wanawake Duniani, wanawake wa Mamlaka huwa tunatembelea wahitaji na kuwafariji kwa kidogo tulichojaliwa. Niwapongeze wanawake wa GCLA kwa kuonesha upendo kwa jamii na kuwaomba kuendeleza tamaduni hiyo", alisema Chiligati.

Aidha, muuguzi kutoka kitengo cha kuhudumia watoto njiti hospitali ya Taifa Muhimbili, Monica Mtundu amewashukuru wanawake wa GCLA kwa kuonesha upendo kwa watoto hao waliopo chini ya uangalizi.

Kwa upande wao wazazi wa watoto waliopo chini ya uangalizi, wameziomba taasisi, mashirika na makundi mbalimbali kujitokeza kusaidia wenye uhitaji iwapo wataguswa.

Sambamba na hayo, wanawake wa Mamlaka wamewalipia gharama za hospitali kwa zaidi ya wazazi 12 waliokuwa wameshindwa kulipa bili za matibabu ili waweze kuruhusiwa.

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 2026, yenye kaulimbiu "Haki sawa kwa Wanawake na Wasichana, Msingi Jumuishi Kufikia Dira ya 2050" kwa Mkoa wa Dar es Salaam yalifanyika kwenye viwanja vya Mburahati Machi 8, 2026.

## GCLA YASHINDA TUZO MBILI MAONESHO YA MADINI GEITA

Mwanaheri Jazza

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeshinda tuzo mbili katika Maonesho ya Nane ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika katika Viwanja vya Maonesho vya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Bombambili mkoani Geita.

Tuzo hizo ni pamoja na tuzo ya Mshindi wa pili kwa Taasisi za Umma za Udhibiti, na Tuzo ya pili ni Tuzo ya Mshindi wa tatu kwa Taasisi wezeshi za Serikali katika Sekta ya Madini.

Tuzo hizo zimekabidhiwa na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said, ikiwa ni sehemu kubwa kwa mchango wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika kutoa elimu ya udhibiti na Usimamizi wa kemikali kwa wadau madini.

Kupitia tuzo hizo Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imethibitisha nafasi yake muhimu katika Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali pamoja na kuwa mchango mkubwa wa sekta hiyo katika pato la Taifa.





# MKEMIA MKUU WA SERIKALI: TAFITI ZETU ZILENGE KUHUDUMIA JAMII - Na Sylvester Omary

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt. Fidelice Mafumiko, ametoa wito kwa watafiti na watumishi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) kujikita zaidi katika kufanya tafiti zenye manufaa kwa jamii, hususan zile zinazolenga kulinda afya za binadamu na mazingira.

Akizungumza Novemba 11, 2025, wakati wa uzinduzi wa Kamati ya Pili ya Utafiti ya Mamlaka uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Mkemia, jijini Dar es Salaam, Dkt. Mafumiko alisisitiza kuwa tafiti ni nyenzo muhimu katika kuchangia maendeleo ya Taifa na kuboresha maisha ya Watanzania.

"Ni wajibu wetu kufanya tafiti kama ambavyo sheria inatutaka, pamoja na kufuata miongozo ya Serikali ili kuchangia utatuzi wa changamoto zinazoikabili jamii," alisema Dkt. Mafumiko.

Alieleza kuwa moja ya majukumu makuu ya GCLA ni kufanya tafiti zenye kuleta manufaa kwa jamii, kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sura ya 177 (Sheria Na. 8 ya mwaka 2016). Pia alikumbusha kuwa utafiti si jambo jipya katika taasisi hiyo, akitolea mfano kuwa ugunduzi wa vimelea vya malaria ulifanyika katika taasisi hiyo, jambo linalodhihirisha mchango wake mkubwa katika historia ya sayansi nchini.

Aidha, Dkt. Mafumiko aliipongeza Kamati ya kwanza ya Utafiti kwa kazi nzuri waliyoifanya, ikiwemo kuandaa taratibu na nyaraka mbalimbali pamoja na kusimamia tafiti zilizochangia kutatua changamoto za kiafya na kimazingira nchini.

Mkemia Mkuu wa Serikali, pia alitoa maagizo mahsusi kwa Kamati mpya kuhakikisha tafiti zote zinazingatia miongozo ya Serikali na kulenga katika kutatua changamoto halisi za jamii na kuandaa maandiko ya tafiti yenye ubora yanayoweza kuvutia ufadhili wa rasilimali.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Utafiti, Dkt. Fidelis Bugoye, alimshukuru Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kuwaamini na kuwateua kushika majukumu hayo. Aliahidi kuwa Kamati itafanya kazi kwa bidii na ubunifu ili kuleta mageuzi katika utatuzi wa changamoto zinazokabili Mamlaka, Wizara na jamii kwa ujumla.

Aidha, aliwataka wajumbe wenzake kudumisha ushirikiano na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu yao kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo ili kufanikisha malengo yaliyowekwa na kuacha alama chanya kwa kamati zitakazofuata.





# GCLA YAENDELEA KUIMARISHA USIMAMIZI WA VINASABA NCHINI - Na Judith Meingarai

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeeendelea kuimarisha uwezo wa usimamizi wa teknolojia za vinasaba nchini kwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi wapya wa Maabara za Vinasaba vya Binadamu hatua ambayo inalenga kulinda usalama wa taarifa nyeti za kibaiolojia na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa kisayansi nchini.

Mafunzo hayo yalifunguliwa rasmi jijini Dar es Salaam, Novemba 20, 2025 na Mkurugenzi wa Huduma za Sayansi Jinai, Bw. David Elias, aliyemwakilisha Mkemia Mkuu wa Serikali. Akizungumza katika ufunguzi huo, alishukuru Serikali kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi katika ukuaji wa sekta ya sayansi na teknolojia na kupongeza waandaaji wa mafunzo hayo kwa jukumu lao la kuandaa programu muhimu na yenye tija kwa taifa.

“Mafunzo haya ni ukurasa mpya katika safari ya kujenga mifumo imara, salama na yenye kuaminika katika huduma za udhibiti wa matumizi ya teknolojia ya vinasaba vya binadamu,” alisema Elias.

Mafunzo hayo yanatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu Na. 8 ya Mwaka 2009 na Kanuni za mwaka 2019, ambazo zinatoa mwongozo wa kuhakikisha kuwa tafiti na uchunguzi wa Vinasaba unafanyika kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma, maadili, haki na usalama wa watumiaji.

Alifafanua kuwa kumekuwa na mwamko mkubwa kutoka sekta binafsi, hospitali, taasisi za utafiti na wadau wengine kuanzisha na kusajili maabara za Vinasaba, jambo linaloonesha mafanikio ya mkakati wa Serikali wa kuwekeza katika sayansi na ubunifu. Hata hivyo, ongezeko hilo linahitaji usimamizi madhubuti ili kulinda maslahi ya taifa, usalama wa raia na heshima ya taarifa nyeti za kibaiolojia.

“Serikali inahitaji mifumo thabiti ya udhibiti, utendaji wenye kasi, uwajibikaji na matokeo yanayoonekana. Ninyi wakaguzi ndiyo injini ya mageuzi haya ya kisera na kitaasisi,” alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Bw. Daniel Ndiyo, alisema kuwa sekta ya Vinasaba inaendelea kupanuka kwa kasi na mahitaji ya wadau yanaongezeka, hivyo kuna umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa shughuli hizo kupitia Kanda badala ya kutegemea Makao Makuu pekee.

“Kwa sasa hatuwezi kuwa na wakaguzi wote katika kila kanda, lakini tumeanza kuwaandaa hawa wachache ili wawe focal persons kwenye maeneo yao na hatimaye wawe wakaguzi walioidhinishwa na kutangazwa kwenye gazeti la Serikali,” alisema Ndiyo.

Naye mwakilishi wa washiriki wa mafunzo, Pascal Mahanju, alitoa wito kwa wakaguzi kujituma na kufuatilia kwa makini masomo yote, ili waweze kuleta matokeo chanya na kuwa msaada katika kuimarisha mifumo ya vinasaba kwenye maeneo yao ya kazi.

“Haya ni mafunzo ya kipekee na ya kimkakati. Tukiyatumia vizuri, tutakuwa sehemu muhimu ya kulijenga taifa lenye uwezo mkubwa katika sayansi ya





Gcla Tanzania/gcla_official/gcla1895
gcla_tv/www.gcla.go.tz/0800116060 (Bure)

# Wasiliana Nasi

Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ipo tayari kuwahudumia wananchi na wadau wote kwa kutoa huduma za kitaalamu, ushauri na taarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala ya maabara, kemikali na uchunguzi wa kisayansi.

Tunawakaribisha kuwasiliana nasi kwa maoni, ushauri, maswali au taarifa kupitia ofisi zetu na njia rasmi za mawasiliano. Ushirikiano wako ni muhimu katika kuboresha huduma na kuhakikisha usalama wa jamii.

Karibu tushirikiane kwa maendeleo na ustawi wa Taifa.





Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
5 Barabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Secherela,
Kata ya Tambukareli,
Kitalu Na 138 & 140,
Kiwanja 'AC'
S.L.P 2925, 41104 Dodoma
Simu: (+255) 0262161630
Barua pepe
gcla@gcla.go.tz